# Nipashe

Ijumaa Januari 24, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580136

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




Ilivyokaa tafsiri benki, chimbuko lake na safari yake ilikofika nchini

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Mapambano ya Takukuru yanapofungua macho ugonjwa sugu wizi ndani ushirika

Habari katika picha

Pata somo la umaskini, tabia zake na namna ya kuukabili

UKURASA 13



## Tanzania yang'ara kimataifa mapambano dhidi ya rushwa

UKURASA 3

# Mwaka mmoja, miezi 7 Lugola Mambo ya Ndani

• **Kipindi** kilichojaa amri, sifa kwa JPM, mrithi wake apatikana, mwenyewe atoa ya moyoni... *Endelea uk.2*



## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**TRA YASIKIA KILIO UKADIRIAJI WA KODI**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema imeboresha mifumo ya kupokea taarifa na uchakataji kwa lengo la kuondoa malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara...

UKURASA WA 7

**WANGWE AMWANGUKIA JAJI MKUU KISA MIL. 5/-**

MKURUGENZI wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Bob Wangwe, amemwomba Jaji Mkuu, Prof. Ibrahimu Juma, kuingilia kati suala lake la kurejeshewa Sh. milioni 5 baada...

UKURASA WA 26

**SHAHIDI KESI KINA MBOWE ADAI KUPIGWA RISASI NA POLISI**

SHAHIDI wa 12 katika kesi ya uchochezi dhidi ya vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiwamo Mwenyekiti...


## Vigogo taasisi za umma wakwepa vitanzi gawio

UKURASA 2

## Wanawake 3 wafa kwa kupigwa na radi

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


**MICHEZO** EYMAEL AFUNGUKA USAJILI MPYA YANGA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais John Magufuli akikagua baada ya kufungua rasmi nyumba za maofisa na askari wa Jeshi la Magereza, Gereza la Ukonga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Mwaka mmoja, miezi saba ya Lugola Mambo ya Ndani

**Na Romana Mallya**

HAKUNA marefu yasiyo na ncha. Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, kufikia ukomo katika nafasi hiyo, baada ya Rais John Magufuli kutangaza kutengua uteuzi wake jana.

Sambamba na Lugola, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu, amejiuzulu wadhifa wake huku Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, akiondolewa kwenye nafasi hiyo.

Lugola ambaye kila alipokuwa akisimama alikuwa lazima amsifie Rais Magufuli kwa kumtaja majina kama 'jembe' na 'jemadari' wamewekwa na kujiweka kando kutokana na kile kilichoelezwa kutia saini mkataba wa makubaliano katika mkataba usio na tija kwa taifa.

Kangi ambaye amedumu ndani ya wizara hiyo takriban mwaka mmoja, miezi sita na siku 23, uteuzi wake ulitangazwa kukoma jana wakati Rais Magufuli akizindua nyumba za makazi za Jeshi la Magereza, Ukonga jijini Dar es Salaam.

Mwanasiasa huyo ambaye kabla ya kuingia kwenye siasa alikuwa ofisa mwandamizi wa Jeshi la Polisi, alishika wadhifa huo Julai Mosi, 2018 kuchukua nafasi ya Mwigulu Nchemba ambaye uteuzi wake ulitenguliwa.

**MRITHI WAKE TAYARI**

Kutokana na kutenguliwa kwa nafasi hiyo, Rais Magufuli amemteua George Simbachawene kuchukua nafasi yake, kabla ya hapo, Simbachawene alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), nafasi ambayo imechukuliwa na Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan Zungu.

Wakati nafasi ya Lugola ikijazwa, aliyekuwa Katibu Mkuu, Jenerali Kingu, ameteuliwa kuwa Balozi pamoja na Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike. Kingu na Kasike watapangiwa vituo vya kazi baadaye.

**KAULI NA VITUKO**

Katika kipindi chote akiwa katika nafasi hiyo akitokea Ofisi ya Makamu wa Rais alikokuwa Naibu Waziri wa Muungano na Mazingira, Lugola alipata umaarufu kutokana na kauli zake, vituko kemkem na kumsifia Rais Magufuli kila alipokuwa akisimama na kuzungumza.

Miongoni mwa kauli zake ni pamoja na maagizo kwa wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara na hata kuchukua hatua dhidi ya baadhi ya maofisa waandamizi kwa kuwatoa katika nyadhifa zao.

Ndani ya siku mbili baada ya kuapishwa, yaani Julai 6, 2018 Lugola alimfukuza kikaoni aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Magereza, Dk. Juma Malewa, kwa kuchelewa kufika kikaoni.

Julai 14, wakati Rais John Magufuli akimwapisha Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike na viongozi wengine, Lugola alipopewa nafasi ya kuzungumza Ikulu jijini Dar es Salaam, alimhakikishia Rais kuwa atapambana na ajali za barabarani.

"Uliponiapisha yapo mambo ya msingi ambayo ulinielekeza niyafanyie kazi. Ninakuhakikishia mambo hayo nimeshaanza kuyafanyia kazi pamoja na makatibu wangu.

"Kwa upande wa ajali tayari tumeshaanza kuchukua hatua na nataka nikuthibitishie utapata usingizi na hata salamu za pole zitapungua na zitakwenda kwisha kabisa ndani ya muda mfupi," alisema.

Lugola pia alimtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, kumpeleka ofisi kwake mmiliki wa Kampuni ya Lugumi Enterprises, Said Lugumi, kutokana na sakata la mkataba tata kati ya kampuni hiyo na Jeshi la Polisi.

Kampuni hiyo ilikuwa inatekeleza mradi wenye thamani ya Sh. bilioni 37 wa kusimika mfumo wa utambuzi wa alama za vidole kwenye vituo vya polisi nchi nzima.

Licha ya kulipwa asilimia 90 ya fedha kwa mujibu wa mkataba, kampuni hiyo ilifunga mashine za kielektroniki katika vituo 14 kati ya 108.

Kutokana na suala hilo kutajwa na Rais Magufuli kuwa ni miongoni mwa mambo ambayo hayakufanyiwa kazi na Mwigulu, Lugola alitoa siku 11 (zilizoishia Julai 31) kwa IGP Sirro kumpeleka ofisini kwake Lugumi na alitii amri hiyo.

Kuhusu mbwa wa polisi, Lugola pia alitoa saa 24 kwa IGP Sirro kuhakikisha mbwa maalum wa Kikosi cha Bandari ambaye alikuwa haijulikani aliko, anapatikana na akipatikana apigiwe simu ili aende kumwona. Siku iliyofuata, aliwaambia waandishi kuwa habari kuwa suala hilo limefanyiwa uchunguzi, uliobaini kuwa yuko kikosini na hakuwa amepotea.

Agizo lingine ni lile alilotoa kwa uongozi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) kuwasilisha ofisini kwake taarifa kamili kuhusu ununuzi wa mtambo wa utengenezaji kadi ghafi ambao bado haujaletwa Tanzania.

Lugola alimtaka Kamishna Jenerali Kasike kuwasilisha mkakati madhubuti na unaotekelezeka na Magereza wa kujitosheleza kwa chakula ili kuipunguzia serikali mzigo wa kulisha wafungwa.

Pia aliwahi kumtaka IGP Sirro kuendelea kuwachukulia hatua askari wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na kuwabambikia wananchi kesi. Sambamba na hilo, alimwagiza Sirro kuwasilisha mikakati ya kuimarisha usalama, ili Watanzania wafanye shughuli za kiuchumi na kijamii kwa saa 24.

Lugola aliwahi kumwagiza Kamishna Jenerali wa Uhamiaji kuhakikisha maofisa wa idara hiyo wa mikoa na wilaya wanafanya kazi kudhibiti wahamiaji haramu kwa sababu ufanisi wao wa kazi utapimwa kwa kuzingatia juhudi zao.

Kwa upande wa Zimamoto,

INAENDELEA UK. 8

# Vigogo taasisi 183 wakwepa kitanzi cha Magufuli gawio

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VONGOZI wa taasisi, mashirika na kampuni 183 kati ya 187, wamenusurika kufukuzwa kazi baada ya kutekeleza agizo la Rais John Magufuli kwa kutoa gawio na michango kwa serikali kiasi cha Sh. bilioni 25.12.

Aidha, taasisi nne zimeshindwa kulipa gawio na michango kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutokuwa na uzalishaji, upya wa taasisi na kampuni nyingine kurejeshwa serikalini kutokana na mwekezaji kutokidhi vigezo vya mkataba wa ubinafsishaji.

Novemba 24, mwaka jana, Rais Magufuli alizitaka taasisi, mashirika na kampuni kuwasilisha gawio na michango ya huduma za jamii ndani ya siku 60 ambazo zilikamilika jana saa sita usiku.

Akizungumza jana katika hafla ya kupokea hundi za gawio na michango, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema agizo la Rais limetekelezwa kwa asilimia 100 na amevunja rekodi kwa kuwa haijawahi kutokea katika historia ya nchi.

"Kwa kweli zoezi hili kwangu halikuwa rahisi sana, nikifikiria uwingi wa idadi ya taasisi, mashirika na kampuni 187 ambazo hazikuwa zimechangia, nilijua kabisa lazima damu ya wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu itanimwagikia, lakini naona hali imekuwa tofauti kabisa," alisema.

Alisema mwenyekiti wa bodi yeyote na mtendaji mkuu husika angekuwa ameonyesha utovu wa nidhamu kwa kukaidi amri ya Rais alikuwa tayari kuwafukuza kazi jana na wangeondoka na aibu kubwa ya kushindwa mbele ya macho ya Watanzania. "Kila siku huwa naeleza kuwa hii kazi ya Waziri wa Fedha ni ngumu, maana fedha nyingi zinahitajika, na kila sekta ili kutekeleza shughuli mbalimbali za serikali za kupeleka maendeleo kwa wananchi," alisema.

Alisema kuongeza ukusanyaji wa mapato na kulipa gawio na michango ya huduma za jamii kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ni njia ya uhakika ya kujitegemea na kuondokana na fedheha ya kutegemea kuomba misaada nje ya nchi.

"Natamani awamu hii ikiisha tuwe tumefikia kukusanya Sh. trilioni mbili kwa mwezi, mwaka 2020 msisubiri Rais atoe maelekezo ndipo muanze kulipa gawio na michango," alisema.

Aliwataka viongozi wa taasisi hizo kuwajibika ipasavyo kuinua utendaji na kulipa gawio ili kuisaidia serikali kutekeleza shughuli za maendeleo.

Alisisitiza kupunguza matumizi yasiyo ya lazima katika mashirika na taasisi kwa kuwa si vyema nchi maskini viongozi wa taasisi kutanua.

Naye Msajili wa Hazina, Dk. Athuman Mbuttuka, alisema Rais alipokea gawio na michango kutoka kwa taasisi, mashirika na kampuni 79 kati ya 266 kiasi cha Sh. trilioni 1.05.

# Tanzania yapanda chati utokomezaji wa rushwa

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imependa kwa nafasi moja juu kwa viashiria vya kutokomeza rushwa duniani kwa mujibu wa kipimo cha kiwango cha rushwa kwa nchi mbalimbali kiitwacho Corruption Perception Index (CPI).

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Taasisi ya Kimataifa ya Uwazi ya Transparency International kuhusu nchi zilizo mstari wa mbele kwenye vita dhidi ya rushwa ambayo hutolewa kila mwaka duniani.

Tanzania imepanda kwa alama moja hadi 37 kati ya alama 100 wakati mwaka jana ripoti iliyotolewa na CPI ilionyesha kuwa ilipata alama 36 kwa mwaka 2018 na 2017.

Kwa mafanikio hayo, ripoti hiyo inasema Tanzania inazipiku nchi jirani za Kenya na Uganda ambazo zote zilipata alama 28 wakati miaka ya hivi karibuni nchi hizo zilipata alama 27 na 26.

Ilisema Rwanda ndiyo imepata alama nyingi zaidi na kuzishinda nchi zote za Afrika Mashariki (EAC) kwa kupata alama 53, ingawa imeshuka kutoka alama 56 ilizopata mwaka 2018.

Ripoti hiyo ilisema katika ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara, Shelisheli ndiyo imeibuka na alama kubwa zaidi kwa kupata alama 61 ikifuatiwa na Botswana iliyopata alama 56 mwaka jana na mwaka juzi.

Nchi zingine za ukanda wa Sahara zilizopanda alama kubwa zaidi kwenye ukanda huo ni Cap Verde iliyopata alama 58 ikifuatiwa na Namibia na Mauritius ambazo zote zilipata alama 52.

Denmark na New Zealand kwa mujibu wa ripoti hiyo zilipata alama 87 zikifuatiwa na Finland (86) na Uswis alama (85) wakati Somalia ikiambulia alama (9) na Sudan Kusini alama (12).

Kwa upande wa kikanda, ripoti hiyo inaonyesha kuwa nchi 14 kati ya 20 zilizofanya vizuri katika tathmini hiyo zinatoka Ulaya ya Mashariki na Jumuiya ya Ulaya ikijumuisha nchi tisa kutoka Jumuiya ya Ulaya pekee.

"Ingawa nchi za Ulaya Mashariki na Umoja wa Ulaya zimekuwa zikifanya vizuri kwenye CPI kwa kupata alama 66 kati ya 100, nchi hizo si kwamba hazina rushwa," ilisema.

Ukiwa na wastani wa alama 43 kwa miaka minne mfululizo nchi za Bara la Amerika zimeshindwa kupata mafanikio katika mapambano ya rushwa kwa mujibu wa ripoti hiyo.

Wakati Canada ndiyo nchi ambayo imekuwa juu kwa muda mrefu ikipata alama 77 kati ya 100, imeporomoka kwa alama nne tangu mwaka jana.

## TRA yasikia kilio ukadiriaji wa kodi

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema imeboresha mifumo ya kupokea taarifa na uchakataji kwa lengo la kuondoa malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wakati wa ukadiriaji wa kulipa kodi.

Imesema imekuwa ikitoa mafunzo ya ukadiriaji kodi kwa wafanyakazi wake ili kumwezesha mfanyabiashara alipe kodi ya biashara yake kwa uhalali.

Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Msafiri Mbibo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati mkutano kati ya wafanyabiashara wakubwa na TRA uliolenga kuboresha uhusiano kati yao.

"Sidhani kama kuna malalamiko ya ukadiriaji wa kodi kubwa kutoka kwa wafanyabiashara... ninachojua TRA tumeboresha mifumo ya kupokea taarifa ili kuchakata vizuri, tumeongeza ubora wa ukadiriaji," alisema Mbibo.

Alisema TRA pia imeweza kuboresha uhusiano na wafanyabiashara wakubwa kwa kuwa nao karibu wakati wote.

Mbibo alisema kwenye kikao hicho TRA iliwafahamisha wafanyabiashara kuhusu marekebisho ya sheria mbalimbali zilizopitishwa hivi karibuni na bunge.

INAENDELEA UK. 8

# Radi yaua wanawake watatu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WANAWAKE watatu wamefariki dunia kwa kupigwa na radi katika maeneo tofauti mkoani Morogoro.

Mmoja alikumbwa na mauti wakati akikinga maji ya mvua nje ya nyumba yake wakati wawili walikuwa wakitoka shambani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema tukio la kwanza lilitokea jana saa 12 asubuhi katika Kijiji cha Kisaki kituoni wilayani Morogoro, ambapo mwanamke mmoja mkulima, Maua Kibamba (22), alifariki dunia wakati akikinga maji ya mvua.

Maua alipigwa radi na kuungua upande wa kushoto wa mwili wake na kufa papo hapo.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutafungwa, tukio lingine lilitokea juzi saa 2 usiku katika Kijiji cha Dunduma, Kata ya Sungaji Tarafa ya Turiani wilayani Mvomero, ambapo wanawake wawili walikufa kwa kupigwa radi wakitokea shambani.

Mutafungwa alieleza kuwa wanawake hao waliungua maeneo mbalimbali kabla ya kufariki.

Mutafungwa aliwataja wanawake hao ni Dativa Nyego(60), mkulima na mkazi wa Kijiji cha Kichangani na Shukuru Samnyau (28), mkazi wa Kijiji cha Dunduma.

Alisema miili yao imefanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya taratibu zaidi za mazishi.

Alitoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari kujiepusha na athari za mvua kubwa zinazoendelea kunyesha ikiwamo kuepuka kukaa chini ya miti mikubwa na maeneo ya wazi ili kupunguza madhara ya radi.

Wakati huo huo Polisi wanawashikilia watu 11 kwa tuhuma za kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu pamoja na kukamata pikipiki tatu zilizodaiwa zilikuwa zikitumiwa na watuhumiwa katika shughuli za utapeli. Mutafungwa alisema watu hao walikuwa wakifanya utapeli katika maeneo ya vijiji vya Rudewa na Msowero wilayani Kilosa na walibainika baada ya upelelezi uliofanywa na jeshi hilo.

Alisema watuhumiwa hao walikuwa wakiwatapeli wananchi wa maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Morogoro na mikoa ya jirani, kwa kuwauzia nafaka hewa ambazo ni mchele, mahindi na maharage kwa kuwahadaa kwamba ni mali ya wizi ambazo zinauzwa kwa bei nafuu.

Alisema watu hao walikamatwa katika misako mbalimbali iliyoendeshwa Novemba mwaka jana hadi Januari mwaka huu.

Waliokamatwa ni Selemani Fadhili (52), Omary Mohamed (30), Limamu Jackson (28), Mussa Manguture (33), Mfaume Omary(33), Hamadi Kassim (20) na Said Shabani (38) wote wakazi wa Rudewa. Wengine ni Christopher Sprian (25), Shauri Mohamed (42), Abdallah Bakari (45) na Abdallah Mussa (24), wakazi wa Kijiji cha Msowero.


LAND O'LAKES VENTURE37 AgResults INNOVATION IN RESEARCH AND DELIVERY

**Wito wa maombi ya kushiriki katika shindano la mradi wa AgResults (AgResults Tanzania Dairy Productivity Challenge Project)**

Kwa niaba ya **Mradi wa AgResults , Land O' Lakes Venture37** inapenda kukaribisha mashirika na taasisi zinazojihusisha na uuzaji na usambazaji wa pembejeo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, kushiriki katika shindano la tuzo ambapo mradi umedhamiria kutumia mfumo wa kutoa motisha kutokana na kuuza pembejeo na kutoa huduma za ugani ili kuongeza wigo wa kutumia teknolojia bunifu, vifaa na mitizamo kwa ajilli ya kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa kutumia pembejeo zilizo bora. Shindano hili litafanyika katika eneo la **Pwani ya Tanzania**, hasa Mikoa ya **Dar Es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro** (bila kushirikisha Wilaya za **Kilombero na Ulanga**)

**Land O' Lakes Venture37** inatoa wito kwa wote wanaotamani kushiriki kutoka kwenye sekta binafsi, taasisi au mashirika ya umma, na taasisi zisizo za kiserikali kushiriki katika mradi.

Wito wa Maombi ya Ushiriki (Request for Proposal – RFA) unaeleza historia, malengo, sheria ya kushiriki shindano hili ikijumuisha fomu ya maombi na taratibu za namna kuomba na mawasilisho. Katika kuwasilisha maombi, kampuni / shirika / Taasisi itakubaliana na masharti ya wito wa maombi ya ushiriki, ikiwa ni pamoja na taratibu za maombi na maelekezo yaliyowekwa.

Tafadhali kumbuka muda uliopangwa kwa ajili ya kupokea/kuwasilisha maombi ni **saa 11:00 Jioni ya Tarehe 28 Februari 2020.** Nyaraka za maombi lazima ziwasilishwe au zitumwe kwa anwani maalumu ya barua pepe ambayo ni **AgResultsTanzania@gmail.com**, kwa kuwasilisha Ofisi za AgResults zilizopo Veterinary Complex;131 Nelson Mandela Road, Dar es Salaam. Tafadhali andika "**Competitor RFA-AgResults Tanzania Dairy Productivity Project**" katika mstari wa somo la barua pepe au kwenye bahasha itakayobeba maombi hayo.

Mradi utapitia maombi yote na kutathimini kulingana na vigezo vilivyowekwa. Wale wote watakaofanikiwa kuchaguliwa watajulishwa na kuelezwa namna ya ushiriki.

**Ndugu mdau,** unahimizwa kuwasilisha maombi kwa wakati ili ujipatie tuzo/motisha na kuchangia maendeleo katika sekta ya maziwa Tanzania. Kama una maswali au maoni tafadhali tuma kwenye barua pepe ifuatayo; **NMrema@landolakes.org.**Tunatanguliza shukrani zetu kwa kwa kutuma maombi ya wito huu kwa wakati na pia tunategemea ushiriki wako katika mradi huu muhimu.

**Pata nakala ya wito wa maombi kupitia:**

https://agresults.org/news-and-blog/10-blog/152-rfa-tanzania-dairy-competitors

215578602

# TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4 092 | 3 521 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12 790 | 12 015 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 33 052 | 33 025 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2 301 | 5 548 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 86 | (48) |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 95 591 | 91 839 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 129 492 | 130 381 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 33 011 | 33 902 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1 000 | 1 000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3 824 | 4 109 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **315 238** | **315 291** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 92 926 | 91 364 |
| 18 | Amana za Wateja | 98 804 | 97 865 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | 25 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3 420 | 5 869 |
| 28 | Madeni | 69 553 | 68 364 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **264 703** | **263 487** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **50 535** | **51 804** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122 954 | 116 014 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (66 472) | (61 839) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (7 012) | (3 433) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1 065 | 1 062 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **50 535** | **51 804** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 10 091 | 7 711 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 19 661 | 21 077 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15 326 | 16 060 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16.0% | 16.4% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.6% | 14.4% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75.5% | 77.4% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 41.1% | 41.4% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82.6% | 82.7% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.3% | 1.2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.0% | 0.3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-19 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10 588 | 11 694 | 42 633 | 48 538 |
| 2 | Gharama za Riba | (4 861) | (5 620) | (19 013) | (22 785) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5 727** | **6 074** | **23 620** | **25 752** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa/ Yaliorejeshwa | 819 | 734 | 2 481 | (1 037) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1 873) | (1 037) | (4 027) | (3 633) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1 429** | **1 493** | **5 426** | **5 926** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 469 | 498 | 1 901 | 1 279 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 812 | 181 | 3 003 | 4 648 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 148 | 814 | 522 | - |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(9 672)** | **(9 189)** | **(34 367)** | **(34 209)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2 741) | (2 376) | (10 878) | (9 940) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (6 931) | (6 813) | (23 489) | (24 268) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(3 570)** | **(1 925)** | **(6 867)** | **(7 200)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (9) | (106) | (145) | (154) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(3 579)** | **(2 031)** | **(7 012)** | **(7 355)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | (320) |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(3 579)** | **(2 031)** | **(7 012)** | **(7 675)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 154 | 158 | 154 | 157 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (1.46) | (0.83) | (0.71) | (780.80) |
| 15 | | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 7 | 7 | 7 | 7 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -4.54% | -2.59% | -2.22% | -2.00% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -27.98% | -17.36% | -13.70% | -11.91% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 135.16% | 121.43% | 118.32% | -107.99% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.43% | 3.06% | 3.54% | 9.88% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-19 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (3 570) | (1 297) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 3 065 | 1 588 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1 780 | 1 054 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2 497 | 2 297 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (27) | (250) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2 473) | (459) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 757 | 507 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (9) | (45) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **2 021** | **3 395** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (170) | (35) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(170)** | **(35)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 1 851 | 3 361 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 112 923 | 109 562 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **114 774** | **112 923** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116 014** | **-** | **(67 756)** | **0** | **1 284** | **1 065** | **50 607** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (7 012) | - | - | - | **(7 012)** |
| Hisa za upendeleo | 6 940 | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1 284 | - | (1 284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122 954** | **-** | **(73 483)** | **0** | **0** | **1 065** | **50 536** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116 014** | **-** | **(69 349)** | **9 118.58** | **1 114** | **1 384** | **58 282** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (7 355) | - | - | - | **(7 355)** |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 9 118 | (9 118) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (170) | - | 170 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (320) | **(320)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **116 014** | **-** | **(67 756)** | **0** | **1 284** | **1 065** | **50 607** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 24-Jan-20 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 24-Jan-20 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 24-Jan-20 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 24-Jan-20 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 24-Jan-20 |

BancABC part of atlasmara

# MINIMUM DISCLUSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50 000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | Free | Free | Free |
| | | | |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20 000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 1 500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50 000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| | | | |
| CURRENT ACCOUNT | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20 000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3 000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 2 000.00 | N/A | N/A |
| | | | |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | TZS 25 000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 6 000.00 | $ 5.00 | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 2 000 000.00 | $ 2 000.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 5 000.00 | $ 10.00 | N/A |
| | | | |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35 000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 3 000 000.00 | $ 3 000.00 | £ 3 000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 100 000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 1 000 000.00 | $ 1 000.00 | £ 1 000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5 000 000.00 | $ 5 000.00 | £ 5 000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20 000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500 000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25 000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10 000 000.00 | $ 10 000.00 | £ 10 000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10 000 000.00 | $ 10 000.00 | £ 10 000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25 000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |

| GENERAL CHARGES | | | |
|---|---|---|---|
| Bankers Cheque | TZS 50 000.00 | $ 25.00 | N/A |
| | | | |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120 000.00 | $ 120.00 | N/A |
| Technical | TZS 60 000.00 | $ 60.00 | N/A |
| | | | |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15 000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 30 000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| 100 leaves | TZS 60 000.00 | $ 60.00 | £ 60.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15 000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25 000.00 | 10% Per Cheque | 10% Per Cheque |
| **Stop Payment Charges** | TZS 60 000.00 | $ 60.00 | £ 50.00 |
| | | | |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | TZS 10 000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | TZS 4 000.00 | $ 3.00 | £ 2.00 |
| Standing Order - Other local bank | TZS 40 000.00 | $ 30.00 | £ 20.00 |
| Amendment | TZS 5 000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| | | | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| - Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| - Cash Deposit at Branch small denominations 500 above 50 | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch small denominations (2,000 and be | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 0.3% Min 1,000 | N/A | N/A |
| With Account Transfers (Internal) | N/A | N/A | N/A |
| - Cheque deposit | Free | Free | Free |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to | TZS 2 500.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 5 | TZS 6 000.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) abov | 0.15% MAX 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3000 Max 200000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 7,500 Max 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| - Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 2%On small denominations* | 2%On small denominations* |
| | | | |
| Account Closure | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account monthly fee | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 5 000.00 | $ 3.00 | £ 3.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80 000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 75 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Reference Letter | TZS 75 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3 000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1 000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | Comm 0.25% Min 50 Max 500 | comm 0.25% min 50 max 350 |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% per qtr min $200 | 1% per qtr min $200 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Nimri, tiba tezi dume iwe nafuu

**TANGU** zama za kale binadamu wamekuwa wakitumia dawa za asili ikiwamo mizizi, majani na magome. Dawa zinazotokana na mimea na wanyama zimekuwa zikitumiwa maliasili nyingine kutoka baharini, ardhi na kwenye miamba kutibu na kupambana maradhi.

Matumizi ya dawa za mimea na wanyama wa asili ni jambo jema na la kiafya linalokubalika zaidi kwani halina athari kwa watumiaji. Hata hivyo, suala la kupata dozi halisi na viwango vinavyohitajika kutibu maradhi au kuyakinga ni jambo ambalo lilikuwa halijawa na mafanikio makubwa katika sekta ya dawa hasa kwenye jamii nyingi za Kiafrika ambazo kukosekana kipimo halisi cha dozi, kunazilazimisha kukimbilia dawa za kisasa au tiba za Kizungu.

Matumizi ya miti ya asili kutibu magonjwa kama tezi dume kunahitaji utaalamu na mkono wa serikali ili kufanikisha utafiti na majaribio ya dawa hizo, hivyo taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Taasisi ya Tiba za Binadamu (Nimri) kuwa inaanza kutumia tiba hizo za asili ni jambo ambalo bila shaka limewagusa na kuwafurahisha Watanzania wengi.

Taarifa ya NIMRI iliyotolewa kwenye mkutano na wanahabari Dar es Salaam wiki hii, inaeleza kuwa taasisi hiyo imepata dawa kutoka kwenye mimea nchini na imejiridhisha kuwa zina uwezo wa kutibu ugonjwa huo na kupunguza nguvu ya saratani ya tezi dume ambayo imekuwa ni janga linaloathiri wanaume wengi.

Tunaipongeza taasisi hiyo kwa kutuaminisha kuwa wataalamu wa dawa za asilia wana uwezo wa kutafuta, kuzijaribu na kuzitambua dawa zinazoweza kutibu tezi dume. Tunawapongeza na wagunduzi wengine wazawa ambao wamefanikisha utambuzi na kuisaidia Nimri kufikia hatua hiyo kubwa kwenye sekta ya dawa.

Tiba zilizotangazwa na taasisi hiyo zinatumia dawa za asilia, ambazo zina umuhimu na upekee kwenye historia ya binadamu na ni mwanzo wa kuiweka Tanzania kwenye ramani ya dunia kuwa miongoni mwa mataifa makubwa kama China ambayo yamekubuhu kwenye utafiti na matumizi ya dawa hizo.

Nchi nyingine ni India yenye tiba ya asili iitwayo 'Ayurveda' wakati Korea ina ' Kampo' ambazo ni tiba asilia zinazotumiwa kutibu maradhi mbalimbali na dawa zake zimesambaa sehemu mbalimbali duniani.

Tunashauri kuwa mwanzo huo wa kugundua tiba asilia za kupambana na tezi dume, ufungue mlango wa kuzitafiti na kuandaa vidonge dawa nyingine za asilia kama zile za kutibu malaria, vidonda vya tumbo na kisukari zinazoelezwa kuwa zinatumiwa mikoani na maeneo mengine mengi nchini.


Hata hivyo, serikali ifanye juu chini kuisaidia Nimri ili kuhakikisha kuwa dawa za asilia zinazozalishwa zinakuwa na gharama ndogo na zinawafikia Watanzania wote kwa bei nafuu hasa kwa wale walioko vijijini.

Upatikanaji wa dawa hiyo uendane na unafuu si kwa tiba pekee bali pia vipimo ambavyo vimekuwa ni changamoto kubwa kwa wagonjwa wa saratani zote ikiwamo hiyo ya tezi dume.

Kama ikiwezekana serikali ianzishe mfuko maalumu wa tiba kwa kuwa ugunduzi wa tiba ya kansa ya tezi dume ni pambazuko jipya katika kutiba kansa nyingine zikiwamo ya kizazi, tumbo, ngozi na matezi.

Ni wazi kuwa Nimri imefungua macho na kuona mbali kuhusu tiba hizo za asili, hivyo jitihada hizo ziende pamoja na kuandaa misitu ya kuotosha miti yenye dawa za kutibu saratani, lakini pia na kuandaa benki za jeni (Genebanks) za mimea hiyo ili zihifadhiwe na kuendelezwa kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mazao ya mkakati, pacha na Tanzania ya Viwanda

Na Sabato Kasika

**KILIMO** ni uti wa mgongo wa taifa na ndiko kwenye ajira nyingi, kutokana na ukweli kwamba ndio shughuli za Watanzania wengi, yakiwamo ya chakula na biashara.

Mbali na kuwa uti wa mgongo wa taifa, kilimo kimepewa kaulimbiu mbalimbali. Hapo tunataja 'kilimo cha kufa na kupona' na 'siasa ni kilimo' hata 'kilimo kwanza' na nyinginezo.

Hizo zote zinaonyesha jinsi gani kilimo kilivyo na umuhimu na sasa serikali imeamua kuyawekea mkakati baadhi ya mazao ya biashara, ili kuhakikisha wakulima wanafaidi jasho lao na yenyewe inapata kodi.

Korosho, pamba, tumbaku, chai na kahawa ni mazao matano ya biashara, ambayo serikali imeyawekea mkazo maalum kuyaendeleza kwa kasi, lengo ni kuongeza pato la wakulima.

Mbali na hilo, serikali imeamua kufanya yawe chanzo cha kuaminika cha malighafi, katika uchumi wa viwanda na inaendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira na fedha za kigeni.

Hatua hiyo inaongeza usimamizi katika uzalishaji wa mazao hayo makuu ya biashara na inatokana na ukweli kwamba, ni kipindi kirefu uzalishaji wake ulishuka kutokana na changamoto kadhaa zilizopo.

Katika orodha hiyo ya vikwazo, inatajwa ni baadhi ya wakulima kuacha kulima kwa kukatishwa tamaa kwa sababu mbalimbali.

Mojawapo ni vyama vya ushirika kutotekeleza vyema wajibu wao, wizi, dhuluma na ushiriki mdogo wa maofisa kilimo kusimamia kilimo hicho kitaalamu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika moja ya hotuba zake, anasema serikali itaendelea kuimarisha vyama vya msingi vya ushirika wa mazao ya kilimo na masoko vinavyozalisha mazao hayo ya kimkakati.

Ninaamini, uamuzi huo wa serikali utakuwa na mafanikio hasa kwa kuboresha kilimo, hatimaye kufikia Tanzania ya Viwanda, kwani vina uhusiano wa moja kwa moja na sekta ya kilimo, sekta iliyoajiri Watanzania wengi.

Lakini hali hairidhishi, watu hao wanatumia zana duni, ambazo ni vyema wakaachana nazo na kutumia teknolojia ya kisasa, ili kuzalishaji malighafi zenye tija kwa ajili ya viwanda mahitaji ya kawaida.

Wakati serikali ikiwa inaendeleza juhudi za kuboresha mazao hayo ya kimkakati, ni vyema navyo vyama vya ushirika kutimiza wajibu inavyotakiwa na pia vitendo vya wizi na dhuluma viachwe.

Maofisa kilimo nao wanapaswa kutimiza wajibu wao inavyotakiwa, kwani baadhi yao wanadaiwa kwamba hawataki kuishi vijijini na wakulima wanakosa huduma zao.

Viongozi wa vyama vya ushirika na maofisa kilimo, mnaopotosha mnahatarisha juhudi za serikali kuimarisha mazao hayo matano. Ni vyema wakachukuliwa hatua mapema.

Jambo la msingi, ni kila upande kutimiza wajibu inavyotakiwa, kwa kutambua nchi inaelekea kuwa ya viwanda, hivyo ni muhimu kuimarisha kilimo kiwe na tija, vinginevyo kitakwama.

Ushiriki wa makundi hayo bila ujanja ujanja, utachangia kuwapo kwa hamasa kubwa kwenye kilimo na hatimaye uzalishaji kuongezeka ingawa kwa kutumia zana duni zilizopo, lakini kutakuwa na manufaa.

Inaumiza kuona, mkulima anajitahidi kuzalisha, lakini mwisho wa siku wananufaika na watu wengine wanashindwa kupata mazao ya kutosha, kwa kukosa ushauri wa wataalamu wa kilimo, wasioenda shamba.

Ikumbukwe, kilimo ni sekta mwajiri wa Watanzania wengi na chakula kikuu cha biashara, hivyo ni muhimu, kujiimarisha kufikia ndoto ya kuelekea maendeleo mwaka 2025 , nchi kufikia uchumi wa kati.

Serikali inatoa kipaumbele katika sekta ya kilimo, hivyo hatua ni kuungwa mkono na wadau wote wa kilimo, ili kiendelee kuwa uti wa mgongo wa taifa, badala ya kuyumba.

Kilimo imara kinategemea wadau kwenye sekta ya kilimo, hivyo asiwepo wa kujitenga kwenye jambo hilo.

Nirudie kwa kusisitiza kuwa malighafi nyingi zinazohitajika katika viwanda, zinatokana na mazao ya kilimo, hivyo suala la uzalishaji wa mazao shambani lina uhusiano wa karibu na viwanda.

HABARI KITAIFA

# Mbarawa aitaka Bodi Ruwasa kijisafisha

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeiagiza Bodi mpya ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kuhakikisha inaondoa madudu ndani ya wakala huo, ikiwamo uzidishaji fedha katika miradi ya maji inayotekelezwa na makandarasi.

Kufuatia hali hiyo, alisema itaanza kutumia 'Force Account' katika ujenzi wa miradi ya maji ili kuzuia ubadhirifu wa fedha za umma.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, wakati akizindua bodi ya wakala huo jijini hapa.

Prof. Mbarawa alisema kumekuwapo na madudu mengi ambayo yanafanywa na watendaji katika utendaji wao wa kila siku, jambo ambalo halikubaliki.

Alisema watendaji wanatakiwa kuwa wazalendo na waadilifu katika utendaji kazi ili kuinua sekta hiyo.

Waziri huyo alisema uzinduzi wa bodi hiyo ukawe chachu ya kuifanya Ruwasa iwe mfano wa kuigwa na bodi nyingine katika utendaji kazi zao za kila siku.

"Naamini bodi hii itakwenda kufanya mabadiliko makubwa na ndio bodi ya kwanza kuzinduliwa katika mamlaka hii," alisema.

Akizungumzia kuhusu utaratibu wa 'Force account', Waziri alisema wataanza kuutumia utaratibu huo kwa ajili ya kuendesha miradi mbalimbali ya maji inayotekelezwa.

"Watu hawaipendi force account kwa sababu ya maslahi yao binafsi, hivyo basi mwelekeo wa wizara tutaanza kutumia kwenye mifumo ya maji," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema anaamini utaratibu huo utakuwa suluhisho ya makandarasi wanaofanya utapeli wa kuongeza fedha katika miradi wanayopewa kufanya katika maeneo mbalimbali nchini.

Naye Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema wataalamu wanapaswa kuelekeza nguvu zao vijijini ili kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya maji.

Alisema watu wa vijijini wamekuwa wakipata shida ya maji, na kunywa maji wanayokunywa wanyama.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ruwasa, Prof. Idris Mshoro, alisema bodi yao ipo tayari kutekeleza maagizo yaliyotolewa na viongozi hao.

# Wangwe amwangukia Jaji Mkuu kisa mil. 5/-

**Na Enock Charles**

MKURUGENZI wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Bob Wangwe, amemwomba Jaji Mkuu, Prof. Ibrahimu Juma, kuingilia kati suala lake la kurejeshewa Sh. milioni 5 baada ya kushinda kesi ya makosa ya mtandao iliyofunguliwa dhidi yake na Jamhuri katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Mei 2016. Wangwe alishinda Machi mwaka jana baada ya kwenda Mahakama Kuu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Wangwe alisema kuwa licha ya kushinda kesi hiyo na kufuata taratibu zote ili kurejeshewa fedha zake, ikiwa ni pamoja na kuandika barua na kuambatanisha nakala ya hukumu na risiti ya malipo kwenda katika Mahakama ya Kisutu ambayo ndio iliyomtia hatiani, lakini mpaka sasa hajarejeshewa fedha zake.

"Ninamwomba sana Jaji Mkuu kuingilia kati suala la fedha hiyo inaweza kuwa ndogo kwa wengine, lakini kwangu ni kubwa sana, na hata kama ni ndogo ninastahili kuipata kwa sababu ni haki yangu," alisema Wangwe. Bob Wangwe alifunguliwa kesi ya kufanya makosa ya mtandao na Jamhuri Mei mwaka 2016 katika Mahakama ya Wilaya ya Kisutu, akidaiwa kusambaza ujumbe uliodaiwa kwenda kinyume cha kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015.

Alisema alitiwa hatiani na Mahakama hiyo na kutakiwa ama kulipa faini ya Sh. milioni 5 au kwenda jela kwa mwaka mmoja na miezi sita. Aidha, Bob alisema alichagua kulipa faini hiyo, huku akikata rufani ya kupinga hukumu hiyo Mahakama Kuu ya Dar es Salaam na baadaye kupewa ushindi Machi 27, mwaka jana, baada ya Jaji Seif Mwinshehe Kulita kusema kuwa alihukumiwa kimakosa kwa kuwa hapakuwa na ushahidi wa kutosha kumtia hatiani ikiwamo kutokuitwa mahakamani mashahidi muhimu waliotajwa katika shauri hilo kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuthibitisha madai dhidi yake.

Akitaja mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kutoa hukumu katika kesi ya makosa ya mtandaoni, Jaji Kulita alisema ni muhimu kuzingatia kuwa ni lazima muhusika (mtuhumiwa) awe ametoa taarifa hiyo yeye mwenyewe, iwe imethibitishwa kuwa ni taarifa ya uongo na pia kama imelenga kuleta taharuki.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi huyo alitoa wito kwa Jaji Mkuu Prof. Juma kupitia upya mfumo wa utoaji haki ili kuharakisha utoaji haki, tofauti na hali ilivyo sasa ambapo alidai pamekuwa na ucheleweshwaji wa utolewaji haki hali inayopelekea haki kwa baadhi ya watu kufungua au kufunguliwa mashtaka mahakamani kupotea.

"Kuna msemo usemao kuwa kucheleweshwa kwa haki ni kunyimwa haki," alisema Wangwe.

Alisema kwa upo umuhimu kwa Jaji Mkuu kutoa tamko la kuruhusu mashauri yote yenye maslahi ya umma kurushwa moja kwa moja katika vyombo vya habari kutokea katika chumba cha Mahakama kama ilivyo katika baadhi ya nchi ili wananchi waweze kufuatilia ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika mhimili wa mahakama.


BONITE BOTTLERS LIMITED

**Advertisements of Employment**

**1. Mechanical Technician**

Qualification:
- Applicant should be a holder of Bachelor Degree /Diploma in Mechanical Engineering from a recognised Institution.

Key skills & Abilities:
- Ability to maintain all the mechanical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation, and to ensure the smooth running of the Line and service equipment by close communication with other staff.
- Ability to operate the machines as directed and to ensure they are running smoothly and efficiently as required and kept clean as required.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated and flexible person and a good team player

**2. Electrical Technician**

Qualification:
- Applicant should be a holder of Bachelor Degree/Diploma in Electrical/Electronic Engineering from a recognized institution.

Key skills & Abilities:
- Ability to maintain all the electrical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation, and to ensure the smooth running of the Line and Service equipment by close communication with other staff
- Ability to operate the machines as directed and to ensure they are running smoothly and efficiently as required and kept clean as required.
- Ability to ensure the correct electrical functioning of all electrically operated machines on the premises.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated and flexible person and a good team player

- Experience : 4 years or above in Mechanical/Electrical field.
- Location : Moshi.

Mode of Application:
All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to the undersigned address to reach him not later than 28/01/2020.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI**

215596302



**TATHIMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII**

**TAARIFA KUHUSU MRADI TARAJIWA WA DHAHABU WA NYAMULILIMA, KWA AJILI YA KAMPUNI YA GEITA GOLD MINING LIMITED, WILAYA YA GEITA, MKOA WA GEITA**

Mradi tarajiwa wa uchimbaji wa dhahabu katika eneo la Nyamulilima upo ndani ya ukanda wa madini wa ziwa Victoria takribani kilometa 20 hadi 25 kwa njia ya barabara kutokea mji wa Geita. Mradi pendekezwa unamilikiwa na kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) ambayo ni kampuni tanzu ya AngloGold Ashanti. Mradi huu upo ndani ya leseni mahsusi ya uchimbaji madini yenye yaani *Special Mining Licence (SML)* namba 45/99 iliyotolewa Juni 1999. Sehemu ya leseni ulipo mradi ipo ndani ya kata Nyamwilolelwa, wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita.

Mgodi wa Geita umekuwa ukifanya uchimbaji wa madini kwa kutumia njia ya mashimo ya wazi na uchimbaji wa chini ya ardhi an uchenjuaji kwa kutumia sayanadi. Hata hivyo, rasilimali ya dhahabu iliyobaki kwa mgodi wa Geita inaonekana kuisha mwishoni mwa mwaka 2020. Hivyo, kwa mgodi wa Geita kuendelea kutoa mchango muhimu katika uchumi wa Tanzania, utafiti ulisaidia kugundua maeneo mengine mbadala ndani ya leseni yenye madini. Maeneo ya Nyamlilima yamethibitishwa kuwa na ukanda wenye hifadhi ya dhahabu ambao utaweza kupatikana na kuingizwa katika uzalishaji kwa kupitia njia ya uchimbaji wa mashimo ya wazi na pengine uchimbaji wa chini ya ardhi hapo baadae.

Hifadhi ya madini ya dhahabu iliyopopo na inayopendekezwa kuchimbwa kutoka eneo la Nyamlilima ni miongoni miradi ya uchimbaji ambayo itasaidia kuendelea kuwepo kwa shughuli za uchimbaji zinazofanywa kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML)hata baada ya mwaka 2020. Ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu, tathmini ya athari za kimazingira na kijamii inahitajika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya usimamizi wa mazingira, 2004 na Sheria ya Madini, 2010.

Pia ili kukidhi mahitaji ya sheria ya mazingira ya taifa na kuhakikisha shughuli zinaendana na viwango vinavyokubalika kimataifa kwa ajili ya usimamizi wa mazingira na mahitaji ya kijamii; kampuni ya GGML imeiteua kampuni ya ushauri iitwayo MTL kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii zinazoweza kutokana na mradii. Utafiti huo utachunguza faida pamoja na athari na kuelezea hatua zote mbadala zitakazotumika ili kuongeza faida na kupunguza athari.

Ili kufikia mahitaji ya kisheria ya ndani ya nchi na yale ya kimataifa katika kufanya utafiti huu wa athari za kimazingira na kijamii, majadiliano na wadau wanaohusika na mradi ni muhimu. Na hivyo tangazo hili linawakaribisha wadau wote wenye maslahi, ushauri au taarifa muhimu kuhusu athari zozote ama za kimazingira au kijamii kuhusiana na mradi huu kuwasiliana kwa simu au kwa kutoa mawazo kwa Msahuri Mwelekezi kupitia anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji**
**MTL Consulting Company Limited,**
**Masaki, Nyumba namba 2,Kitalu 689,**
**S.L.P 77894, Barabara ya Sandvik**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel./Fax: +255 22 2600594**
**Cellular: +255 (0) 767 360 225**
**Email: emasasila@mtlconsulting-tz.com**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**
**S.L.P 63154, Regent Estate Plot No. 29/30,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255 22 2774889**
**Email: dg@nemc.or.tz**

215596502

# Mwaka mmoja, miezi saba ya Lugola Mambo ya Ndani

INATOKA UK. 2

aliagiza askari wa jeshi hilo kuhakikisha askari wake wanafika kwenye matukio badala ya kutoa kisingizio cha kutokuwa na magari ya kuzima moto.

Agizo lingine kwa IGP Sirro alimtaka ampelekee orodha ya miaka mitano ya matukio ya utekaji wa bodaboda na kuuawa madereva wake ili kutafuta mwarobaini wa matukio hayo.

Aliwahi kusema kuwa siku za mtu mmoja anayejitambulisha kwa jina la Kigogo mtandaoni, zinahesabika.

**SIFA KWA RAIS**

Kama ilivyo ada kumsifia Rais, jana, Lugola alipopewa nafasi ya kuzungumza katika uzinduzi wa nyumba za Jeshi la Magereza alisema ilani ya CCM ibara ya nne, wakati Rais akizunguka nchini aliwaahidi wananchi kwamba itahakikisha amani, usalama na utulivu.

"Uliwahakikisha wananchi pamoja na mali zao zitalindwa kwa nguvu zote za serkali naomba nithibitishie umma, moja wapo ya wizara ulizoundwa kutekeleza amani, usalama na utulivu ni Wizara ya Mambo ya Ndani.

"Tukiwa tunawaambia na kuwathibitishia Watanzania pamoja na kwamba tuna muda mfupi wa kumaliza miaka mitano, lakini Dk. John Pombe Magufuli ametekeleza ilani hii kuhakikisha nchi hii imetulia mahali pake.

"Kulikuwa na matukio ya ujambazi wa kutumia bunduki leo ni historia wananchi wanalala bila kusikia milio ya bunduki, kulikuwa na ajali nyingi ukatuhimiza tukasema hatutakuangusha, ajali zilizokuwa zinachukua uhai na mali zao, zinaishia ukingoni."

"Kumekuwa na maneno kwamba fedha ambazo unawaambia watu unakusanya kwa ajili ya nchi hii na kwamba umeipaisha kwenye uchumi, wapo watu wengine pamoja na wanaona, lakini hawataki kukubali matokeo.

"Nataka niwahakikishie ibara 146 katika ilani hii uliwahakikishia Watanzania vyombo vya ulinzi na usalama kwa ajili ya kujenga ari ili kulinda nchi."

Alimweleza Rais Magufuli kuwa kama kuna wakati amevisaidia vyombo vya ulinzi na usalama kwenye eneo la makazi ni kipindi chake.

"Ndiyo maana vyombo vya ulinzi na usalama kila kukicha majengo ambayo unatupa fedha, tunakuwa na majengo ya Uhamiaji, Zimamoto na leo ya Jeshi la Magereza.

"Walikuwa na majengo duni tangu mkoloni tangu alipoliacha Jeshi la Magereza halikuwahi kuwa na nyumba hata moja ya ghorofa, leo umetujengea maghorofa na kuandika historia.

"Zilitolewa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa makazi, lakini TBA walipokuja hapa hatukuweza kutimiza azma hii naamini



George Simbachawene

alikuja shetani na jeshi lake akakalia hapa, ndiyo maana TBA wakawa na kigugumizi kwa sababu walipigwa upofu, ulipotinga hapa na majeshi wawili, jeshi la Mungu na la ulinzi la JKT, wakakimbia na matokeo unatukabidhi nyumba hizi.

"Wanaobeza na wanaona macho yao hayaoni tunawaambia siku za serikali ya awamu ya tano zinafikia mwisho Watanzania wanaokuunga mkono ni 99.1 hako kaasilimia 0.1 ni hao walioshikiliwa na shetani, lakini washindwe walegee nafungua minyororo na upofu ili wakukubali kwa kuwa kipindi hiki umewekwa juu utaendelea kung'ara."

**KAULI BAADA YA KUONDOLEWA**

Lugola alisema Rais Magufuli ndiye aliyemteua Baraza la Mawaziri na ndiye aliyeona ampumzishe.

"Kwangu ni jambo la faraja na hata nyinyi Watanzania vikiwamo vyombo vya habari mmesikia hatua alizochukua ni hatua nzuri zinalenga kujenga safu ya serikali, ninaahidi kwamba kama mbunge niliyepata nafasi ya kumsaidia Rais nitaendelea kumsaidia kutumikia serikali awamu ya tano kwa heshima kubwa," alisema.

**MADUDU YA WIZARA**

Rais Magufuli alifunguka jana kuwa na kusema kazi ya uongozi wakati mwingine ni mgumu, ziko changamoto nyingi hasa katika wizara hiyo.

"Kama kuna wizara inanitesa ni hii, ninataka Watanzania wanielewe, inanitesa sana, Mheshimiwa (Mussa) Zungu (Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama) atakumbuka tangu tumeingia madarakani katika kipindi cha miaka minne, kuna tume nyingi zimeundwa kwa ajili ya kuchunguza wizara hii.

"Kuna miradi ya ovyo iliyokuwa ikifanyika, nilitegemea watu wangekuwa wanajifunza ninajua Waziri wa Mambo ya Ndani haonekani hapa, ameshaleta barua ya kujiuzulu na nimemkubalia, nimempongeza kwa kutambua hilo," alisema.

**AFICHUA YALIYOMO**

Rais Magufuli alisema, "Kitu kikubwa ni nini, watu kukosa uadilifu, hivi karibuni kulikuwa na mkataba mmoja wa ajabu unatengenezwa Wizara ya Mambo ya Ndani wenye thamani ya Uero milioni 408 (zaidi Sh. trilioni moja).

"Mradi umetayarishwa na kusainiwa na Kamishna wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, haujapangwa kwenye bajeti haujapitishwa na Bunge.

"Wakati wa vikao na kampuni moja nafikiri kutoka Romania wahusika wote wa Tanzania walipokuwa wanakwenda kwenye majadiliano wanalipwa posho ya kikao dolla 800 (sawa na Sh. milioni 1.8) bado kulipiwa tiketi ya ndege, mradi wa ovyo.

"Wamesaini makubaliano ya pamoja, lakini ukitaka kuyavunja makubaliano hayo ya ndani yale ambayo yameanza kutekelezwa lazima yaendelee kutekelezwa.

"Lugola nampenda sana ni mwanafunzi wangu nimemfundisha Sengerema, pamoja na mwili wake ni mwanafunzi wangu, lakini kwenye hili hapana, nilitegemea hata hapa nisingemkuta, nasema kwa dhati.

"Kamishna Jenerali Andengenye nampenda sana ni mchapakazi lakini kwenye hili hapana. Nilitegemea hapa awe hayupo. Hatuwezi kuendesha nchi kwa misingi ya ajabu namna hii."

Rais Magufuli alisisitiza kuwa yanayokwenda kununuliwa kwenye mkataba huo ni ya ovyo na ajabu.

"Ndiyo maana ninasema nina mpongeza sana Meja Jenerali Jacob Kingu ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa wizara hii kwa kuwajibika na hii imempa heshima kwamba angalau ametambua kwamba inawezekana haya hakuyafanya lakini yeye ni Katibu Mkuu, amewajibika kwenye hilo, ninampongeza sana na nitaendelea kumheshimu, kama Meja Jenerali," alisema.


TAARIFA KWA WATEJA

BW. MICHAEL BILDAD MINJA



Tunapenda kuwafahamisha wateja wetu na umma kwa ujumla kuwa mtajwa hapo juu aliajiriwa na Benki ya NMB mnamo tarehe 01 Septemba 2008.

Kuanzia tarehe 20 Januari 2020, sio mwajiriwa wa Benki ya NMB. Tunawatahadharisha wateja wetu na umma kwa ujumla kutojihusisha na mtu huyu kwa masuala yoyote yanayohusisha benki ya NMB. Benki haitawajibika kwa muamala au makubaliano yoyote yanayomhusisha Bw. Michael Bildad Minja.

Imetolewa na: MENEJIMENTI YA NMB


# TRA yasikia kilio ukadiriaji wa kodi

INATOKA UK. 3

Aidha, alisema vigezo vinavyotumika kuwatenganisha wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa ni mapato ghafi yanayozalishwa na mfanyabiashara, viwango vya ajira vinavyotolewa na mfanyabiashara.

Alisema kwa nchi zinazoendelea kutoka kipato cha kati kwenda cha juu kama vile Tanzania, suala la ulipaji kodi ni muhimu na linapaswa kupewa kipaumbele.

Naye Kamishna wa TRA Kitengo cha walipa kodi wakubwa, Alfred Mlegi, alisema kitengo cha walipa kodi wakubwa kinafanya kazi na sekta zote za uchumi kama vile madini, mafuta na gesi, benki, kampuni za simu, hospitali, viwanda, wasafirishaji na mashirika makubwa.

Alisema awali walikuwa na walipakodi wakubwa 395, na kwamba hadi unafanyika mkutano huo idadi iliongezeka na kufikia 504. "TRA ina lengo la kukusanya kodi Sh. trilioni 19.1 kwa mwaka, wafanyabiashara wakubwa tumewawekea lengo la kukusanya Sh. trilioni saba hadi tisa, hivyo ni lazima tukaonao tujadiliane," alisema Mlegi.

Alisema kikao hicho kati ya TRA na wafanyabiashara wakubwa kitaongeza wigo wa ukusanyaji mapato na kufikia lengo lililowekwa na serikali.

Alisema TRA imekuwa na uhusiano mzuri na wafanyabiashara wakubwa na ndiyo sababu makusanyo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka.

HABARI KITAIFA

# Waziri agoma kufungua machinjio ya Msalato

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amegoma kufungua machinjio ya Msalato yaliyopo jijini hapa baada ya kubaini upungufu wa hali ya usafi wa mazingira na ukarabati wa majengo kuwa chini ya viwango.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ziara katika machinjio hayo, Waziri Simbachawene alisema amefikia uamuzi huo baada ya kubaini upungufu mwingi ikiwamo ukarabati kufanyika chini ya kiwango na pia kutozingatia usafi wa mazingira katika eneo hilo. "Natoa wiki moja kuhakikisha mkandarasi anafanya marekebisho ya machinjio haya na pia iandaliwe taarifa ya gharama za ukarabati ili tuweze kufanya tathmini ya kilichofanyika na gharama halisi iliyotumika," alisema Waziri Simbachawene ambaye aliambatana na maofisa kutoka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Alisema ni muhimu kujiridhisha na kujua gharama iliyotumika kukarabati miundombinu hiyo muhimu na kama vinashabiana na fedha ya Watanzania ambayo imetumika katika kazi nzima ya ukarabati.

"Watendaji serikali ni lazima kuwa makini katika kusimamia miradi ili ifanyike kwa ubora stahiki sambamba na thamani ya fedha zinazotumika ambazo ni za walipa kodi," alisema na kuongeza kuwa Watanzania wana imani na matumaini makubwa na utendaji wa serikali ya Rais John Magufuli.

Aliongezea kuwa kilichofanyika katika machinjio hayo kinakinzana na suala zima la utunzaji wa mazingira kwani ujenzi haupo katika mpangilio ambao utayafanya mazingira ya machinjio kuwa katika hali ya usafi na kwa ustawi wa mazingira.

"Sina uhakika kama ujenzi wa machinjio haya umezingatia tathmini ya athari kwa mazingira kwa sababu ujenzi wake haupo katika mpangilio mzuri," alisema Waziri Simbachawene.

Alisema ziara yake ilikuwa ni kufanya ukaguzi ili kujiridhisha kama ujenzi ulifuata kanuni za mwongozo wa utunzaji wa mazingira kwani ni mwaka moja sasa tangu Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira kuifunga machinjio hiyo kwa kuwa haikuwa katika hali salama.

Diwani wa eneo hilo la Msalato, Ali Mdende Mohamed, alikiri udhaifu uliopo na kuahidi yeye na viongozi wenzake watahakikisha kasoro zote zinarekebishwa kwa wakati.

"Tumejipanga kuhakikisha kasoro zote za ujenzi zinarekebishwa na taarifa ya gharama inapatikana kama alivyoagiza Waziri," alisema Mohamed na kuongezea kuwa ukarabati utafanyika ili kuruhusu biashara ziendelee katika machinjio hayo.

Kwa upande wao vijana ambao wanaopata riziki katika machinjio hiyo iliyofungwa kwa baada ya kutishia afya za walaji, wakatoa kilio kwa viongozi kuwajibika, ili machinjio ifunguliwe na wao waendelee kupata kipato. Emmanuel Daniel alisema kufungwa kwa machinjio hiyo kumeathiri shughuli za kiuchumi kwani biashara zimesimama kwa muda.

Mchinjaji katika machinjio hayo, Josephat Chiwanga, aliomba uongozi wa machinjio hayo kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni na taratibu ili kuondoa sintofahamu zisizo za lazima kwa afya bora watu.



Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkuu wa Wizara ya Afya, Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Matias Haule, akitoa ufafanuzi kuhusu maambukizi mapya ya Ukimwi, kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Bicha, iliyoko Kondoa Mjini, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: MAELEZO**

# WB yapiga jeki ukuaji soko mikopo nyumba kwa bil. 13/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Dunia kupitia Shirika lake la Fedha (IFC), ambalo ni mojawapo ya taasisi zisizo za benki hiyo, imetangaza kuwa imeingia ubia na kampuni ya mikopo ya Nyumba Tanzani-TMRC kwa kuwekeza kwa muda mrefu kiasi cha dola za Marekani milioni 5.75 (shilingi bilioni 13.3) kwa ajili ya kuwezesha ukuaji wa soko la mikopo ya nyumba za makazi Tanzania.

Lengo pia ni kuwezesha upatikanaji wa nyumba za makazi za gharama nafuu. Uwekezaji huo unahusisha IFC kununua hisa za TMRC zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.5 ambazo zimelipiwa kwa shilingi za Kitanzania na pia kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 4.25 zitakazotolewa ambazo zitatumika kuwezesha TMRC kutoa hatifungani zake kwenye soko la mitaji la Tanzania kwa muda wa miaka mitano.

Uwekezaji huu wa IFC umewezeshwa na dirisha la sekta binafsi linalotumia fedha zilizotengewa/idhinishwa kwa nchi husika kwa ajili ya uwekezaji.

Jumoke Jagun-Dokunmu, Mkurugenzi wa IFC Kanda ya Afrika Mashariki, alisema kuwa IFC imejipanga kuwezesha ukuaji wa soko la nyumba hapa Afrika kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha za ndani za muda mrefu ambazo ni muhimu kwa ukuaji wa masoko ya nyumba. "Kwa IFC kuwekeza TMRC, IFC inategemea kuongeza kasi ya ukuaji wa soko la nyumba za gharama nafuu Tanzania."

TMRC ni taasisi ya fedha iliandzishwa mwaka 2010 ukiwa ni utekelezaji wa mradi wa serikali ya Tanzania wa mikopo ya nyumba uliofadhiliwa na Benki ya Dunia na inasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa niaba ya serikali.

Benki ya Dunia kupitia BoT ilitoa fedha za uendeshaji za awali kiasi cha dola za kimarekani zipatazo milioni 70 kwa ajili ya kuwezesha TMRC kutoa mikopo kwa benki kwa ajili ya kuziwezesha kukopesha wateja wake mikopo ya nyumba za makazi kwa muda mrefu.

# Hukumu kesi ya kubaka mtoto Jan. 27

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma Mkoa wa Kigoma imeahirisha hukumu ya kesi inayomkabili mganga wa kienyeji Venas Edward (48) mkazi wa Ujiji Manispaa ya Kigoma/Ujiji ambaye anakabiliwa na shtaka moja la kumbaka mtoto wa mwenye umri wa miaka 8.

Mshtakiwa huyo ambaye yuko nje kwa dhamana, alipandishwa kizimbani juzi mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Katoki Mwakitalu ambaye aliahirisha kesi hiyo kwa madai kuwa hukumu haijawa tayari.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Raymond Kimbe, ulidai kuwa kesi hiyo inakuja kwa ajili ya hukumu na upande wa mashtaka uko tayari kusikiliza hukumu hiyo.

Hakimu Mwakitalu alidai mahakamani kuwa hukumu hiyo haijawa tayari na kudai kuwa anaiahirisha kesi hiyo na hukumu hiyo itakuwa tayari Januari 27, mwaka.

Katika kesi hiyo upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi wanne na kielelezo kimoja ambacho ni PF3. Na upande wa mshtakiwa alijitetea pamoja na mashahidi wake watatu.

Awali akisoma maelezo ya awali, Wakili Kimbe alidai kuwa Aprili 23, mwaka 2019 majira ya asubuhi eneo la Kasoko Ujiji Mkoa wa Kigoma, mtoto huyo ambaye jina lake limehifadhiwa, alipelekwa na mama yake nyumbani kwa mshtakiwa ambaye ni mganga wa kienyeji kwa ajili ya matibabu.

Raymond alidai baada ya kufika kwa mshtakiwa huyo alimtuma mama wa mtoto huyo aende dukani kununua wembe, na kuwa mshtakiwa alibaki na mtoto nyumbani kwake.

Aliendelea kudai kuwa baada ya mganga huyo kubaki na mtoto ndipo alipopata nafasi ya kumbaka mtoto huyo, na baadaye mama wa mtoto alifika kutoka dukani kununua wembe na kumchukua mtoto wake na kurudi nyumbani kwake.

Aidha, wakili huyo wa serikali aliendelea kudai kuwa baada ya muda alisikia mtoto analalamika kusikia maumivu sehemu zake za siri, ndipo mama yake alipomkagua na kugundua kuwa mtoto wake amebakwa.

Kimbe alidai kuwa mama wa mtoto huyo alimbana mtoto wake kwa kumuuliza ni nani aliyekufanyia kitendo hicho, na kumtaja mganga huyo wa kienyeji.

# Waziri Kairuki: Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

SERIKALI imewahakikishia wawekezaji katika sekta ya viwanda mkoani Pwani kuwa imejipanga kutatua kero na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo ili kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Akizungumza hivi karibuni katika ziara yake kwenye kiwanda cha mifuko cha Global Packaging kinachomilikiwa na Mtanzania, Joseph Wasonga,

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, mbali ya kuridhishwa na uzalishaji wa bidhaa zenye viwango katika kiwanda hicho, serikali inazifanyia kazi changamoto mbalimbali ikiwamo urasimu kutoka kwa baadhi ya watendaji sekta ya umma na miundombinu.

"Mpo vizuri kwa kuunga mkono kwa dhati juhudi za serikali ya kujenga uchumi ulioimara na unaotegemea viwanda na pia kuzalisha ajira kwa Watanzania na kulipa kodi za serikali," alisema Kairuki.

Kairuki alisema serikali inatambua umuhimu wa wawekezaji na hivyo imekuwa ikiwahamasisha kuwekeza zaidi katika sekta mbalimbali ya uchumi ikiwamo viwanda na kuwahakikishia mazingira bora ya kuwekeza na kufanya biashara. Waziri aliezwa jinsi kiwanda kinavyofanya kazi na jinsi kinavyochangia kodi mbalimbali za serikali na pia alipata nafasi ya kutembelea kuona uzalishaji na kuongea na menejimenti ya kiwanda hicho.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wawekezaji katika kutatua changamoto wanazokabiliana na kuhamasisha Watanzania wengi wenye mitaji kuhamasika kuweka nchini ili kukuza uchumi na maendeleo kwa taifa.

"Serikali imekuwa ikifanya jitihada za mara kwa mara kukutana na wawekezaji na wafanyabiashara kujadiliana nao ili kuboresha mazingira ya uwekezaji hali itakayosaidia kufanikisha azma ya kujenga uchumi wa kati na viwanda kama ilivyopangwa ," alisema Kairuki.

Akielezea utendaji wa kiwanda na mikakati mbalimbali waliyojiwekea Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Benno Mwitumba, alimwambia Waziri kuwa Bodi na Menejimenti ya kiwanda ina imani kubwa sana na serikali kwa kujenga mazingira bora ya uwekezaji hapa nchini na kupongeza hatua mbalimbali zinazofanywa kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

"Ujenzi wa bwawa kubwa la kufua umeme la Mto Rufiji ambalo litazalisha megawati 2,115 za umeme na ujenzi wa reli ya kisasa inaonyesha dhamira ya dhati kuwa serikali imeamua kuleta mageuzi ya makubwa kati uchumi," alisema Mwitumba.

Mwitumba alisema kukamilika kwa ujenzi wa bwawa la umeme kutaondoa tatizo la nishati ya umeme viwandani na pia reli ya kisasa itasaidia usafirishaji wa bidhaa kwa urahisi hali itakayochochea ukuaji wa biashara, hivyo aliwaomba Watanzania kumuunga mkono Rais Dk. Magufuli katika kufanya mageuzi ya uchumi.

"Sisi kama Global Packaging tunatambua juhudi hizo hivyo tutaendelea kuzalisha bidhaa zenye ubora na zinazokidhi ushindani soko la ndani na nje ya nchi," alisema Mwitumba na kumpongeza Waziri Kairuki kwa kuwatembelea wawekezaji na kusikiliza matatizo yao.




Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, Jokate Mwegelo (katikati), akifanya mahojiano na Mtangazaji wa East Africa Television, Deogratius Kithama (kulia), baada ya kupokea taulo za kike kwa ajili ya wanafunzi katika shule mbalimbali kupitia kampeni ya Namthamini inayoendeshwa na EATV/Radio, kwa mwaka wa nne mfululizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kesi ya 'Tereza' yapigwa kalenda

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma Mkoa wa Kigoma, imeahirisha kesi inayomkabili mkazi wa Gungu Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Joseph Richard (25) ambaye anatuhumiwa kuwa mmoja wa wahalifu wa kikundi cha 'Tereza' kwa maelezo kuwa hakimu, Eva Mushi, anayesikiliza kesi hiyo anaumwa.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na shtaka moja la kumshambulia Mwamini Hussein kwa kumkata na panga sehemu za kichwani na kwenye mguu, na kumsababishia majeraha.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani jana akitokea mahabusu katika Gereza la Bangwe na kupandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Katoki Mwakitalu.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clement Masua, alidai kuwa kesi hiyo imekuja kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali na yuko tayari kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo hayo.

Hakimu Mwakitalu alisema anaiahirisha kesi hiyo kwa sababu hakimu mhusika anaumwa, kuipanga Februari 3, mwaka huu.

Alisema mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu hadi hapo atakapopata mdhamini na upande wa mashtaka ujitahidi kuandaa maelezo ya awali tarehe hiyo.

Awali Hakimu Mushi aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa ya mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 2.

# Wakulima wa tumbaku Geita sasa walilia soko

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

WAKULIMA wa tumbaku wilaya za Mbogwe na Bukombe mkoani Geita, wameiomba kampuni ya usambazaji wa pembejeo za kilimo ya Petrobena kununua zao hilo kwenye vyama vya msingi vitatu.

Vyama hivyo ni Mzalendo Kazibizyo, Idoselomwalo na Namsingili vilikosa wanunuzi baada ya kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco Company Limited (TLTC), kusitisha ununuzi wa zao hilo msimu uliopita.

Ombi hilo lilitolewa jana na wakulima wa zao hilo katika kikao cha pili cha Mkutano Mkuu wa Chama cha Ushirika Mbogwe na Bukombe (MBCU) kilichofanyika wilayani Mbogwe mkoani Geita na kuhudhuriwa na Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dk. Titus Kamani.

Catherin Augustino ni wakulima wa zao hilo kutoka Bukombe alisema mpaka sasa vyama hivyo vimeshindwa kupata pembejeo za kukatia vikonyo kwenye tumbaku ikiwamo kukopeshwa na taasisi za kifedha baada ya kufunga mikataba na makampuni yasiyoua na ofisini Mbogwe au Bukombe.

"TLTC ndiyo iliyokuwa inanunua tumbaku yetu na tangu imeondoka tumekata tamaa ya kuendelea kulima zao hili. Kampuni ambazo tumeingia nazo mikataba zimeshindwa kukopesheka na taasisi za kifedha kwa madai hayana ofisi hapa Bukombe na kufanya sisi kukosa pembejeo za kukatia vikonyo," alisema Augustino.

Aliongeza: "Mwenyekiti taarifa tulizonazo Petrobena amefunga mkataba wa kununua tumbaku na Amcos ya Ngokolo chini ya chama kikuu cha ushirika Kahama (Kacu) kwa msimu wa 2019/20, wanashindwa vipi kufunga mikataba kwenye vyama hivi vitatu ili navyo vipate wanunuzi wa uhakika."

Naye Johari Juma alisema kama Petrobena wameweza kusambaza pembejeo kwa wakulima wote kwa wakati unaotakiwa na kuondoa urasimu uliokuwapo hapo awali, wanashindwa vipi kununua tumbaku au pamba kwenye msimu 2019/20.

Akijibu maombi hayo, Dk. Kamani alisema serikali itahakikisha inatatua kero za wakulima hasa za masoko na mwaka huu vyama vyote vilinavyolima tumbaku zimepata wanunuzi.

Aidha, aliwataka viongozi wa Amcos na ushirika kuhakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya maandalizi ya ununuzi wa pembejeo katika msimu ujao, ili kuondokana na mikopo kutoka taasisi za kifedha ambayo imekuwa na riba kubwa.

Kwa upande wake Ofisa Kilimo na Ushirika wa Wilaya ya Mbogwe, Samuel Makala, alisema asilimia 95 ya wakazi wa Mbogwe ni wakulima wa mazao mbalimbali, lakini hawataki kutumia mbolea kwa kisingizio zinaharibu rutuba ya ardhi.

# Mvua yakosesha makazi kaya 16

**Na Allan Isack,** BABATI

KAYA 16 katika Kijiji cha Ngarenaro, Kata ya Galapo, Babati mkoani Manyara, hazina makazi baada ya mvua kubwa iliyonyesha ikiambatana na upepo mkali kuezua mabati na kuharibika mazao mashambani.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wameomba hifadhi kwa muda kwa majirani.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Salum Juma, akizungumza juzi na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alisema wamepoteza makazi yao baada ya kunyesha juzi kwa mvua kubwa iliyoambatana na upepo.

Juma alisema mvua hiyo ilinyesha juzi usiku na kusababisha madhara hayo lakini wanamshukuru Mungu hakuna mtu aliyepoteza maisha.

Alisema mvua hiyo imesababisha madhara kwa wananchi hao kwa kuwa hadi sasa hawafahamu hatima ya maisha yao.

Mbunge wa Babati Vijijini, Vrajlal Jituson, alisema wananchi hao wamepata majeraha kutokana na kuangukiwa na matofali wakati wa dhoruba hiyo.

Jituson alisema katika tukio hilo, miundombinu ya barabara imeharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Kata ya Galapo.

"Tunashukuru viongozi wa serikali kwa kuwa karibu na wananchi baada kutokea kwa tukio hilo. Pia tunawapongeza (Wakala wa Taifa wa Barabara) Tanroads na (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini) Tarura kwa kufika kwa wakati kwenye maeneo hayo," alisema Jituson.

Mkuu wa Wilaya, Kitundu, na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Babati, walitembelea eneo hilo na kutoa pole kwa wananchi waliokumbwa na adha hiyo.

Kitundu na kamati hiyo walikagua na kufanya tathmini ya uharibifu wa nyumba na mazao yaliyoharibika mashambani.



Waendesha bajaji wilayani Bariadi, Mkoa wa Simiyu, wakiwa wamegoma kuendelea na shughuli zao kwa kile walichodai kuwekewa mipaka ya kusafirisha abiria ndani ya wilaya hiyo, jana. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Mwanafunzi asombwa na maji akiogelea

**Na Allan Isack,** BABATI

MVUA zinazoendelea kunyesha mkoani Manyara, zimesababisha madhara baada ya mwanafunzi wa darasa la nne wa Shule ya Msingi Sinai wilayani Babati, kusombwa na maji kwenye Daraja la Mrara.

Mwanafunzi huyo, Salim Muhazar (12), alisombwa na maji juzi mchana akiwa na wenzake watatu walipokuwa wakicheza katika mto wa eneo hilo.

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji mkoani Manyara, Julishael Mfinanga, alisema jana kuwa askari wa jeshi hilo, bado wanaendelea na shughuli ya kutafuta mwili wa mtoto huyo.

Alisema wazamiaji wa jeshi hilo, walimtafuta kwenye kina kirefu walichohisi labda angekuwa amenasa kwenye tope, hawakufanikiwa kumpata na kazi ya kumtafuta ilifanyika hadi kufikia kwenye daraja la Mto Kiongozi.

Hata hivyo, alisema watoto watatu waliokuwa na mwenzao wakati wakiogelea walitoka majini, lakini huyo mmoja alisombwa na maji na mpaka sasa mwili wake haujaonekana.

Pia alisema bado wanaendelea na shughuli ya kutafuta mwili wa mtoto huyo kwa kushirikiana na wananchi mbalimbali wa eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alisema shughuli ya utafutaji wa mwili wa mtoto huyo inaendelea hadi upatikane na kufanyiwa maziko.

Alisema Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Polisi na vyombo mbalimbali vya usalama kwa wakishirikiana na wananchi, wanaendelea kutafuta mwili huo.

Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Gekul, aliwashukuru viongozi wa serikali, taasisi na wananchi wote waliojitokeza kusaidia kutafuta mwili huo.

Gekul alisema wananchi wa eneo hilo, wanakutana kwenye Daraja la Mrara kila asubuhi ili kutafuta mwili wa mtoto huyo.

# Bavicha yakomalia tume huru uchaguzi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

BARAZA la Vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) (BAVICHA) Mkoa wa Arusha, limeitaka serikali kuunda tume huru ya uchaguzi kabla ya uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Arusha katika ofisi za Kanda ya Kaskazini za chama hicho juzi, Mwenyekiti wa Bavicha Mkoa wa Arusha, Emma Kimambo, alisema suluhisho pekee la kuondoa kasoro na malalamiko katika uchaguzi mkuu ni kuwa na tume huru ya uchaguzi.

Kimabo alisema Chadema imekuwa mwathirika wa uchaguzi mbalimbali kwa muda mrefu na kwamba wana kumbukumbu ya matukio yaliyotokea katika uchaguzi ikiwamo wafuasi wao kupigwa, matokeo ya uchaguzi kubadilishwa na masanduku kuporwa ndani ya kituo cha kuhesabia kura.

Alisema kasoro hizo zimekuwa zikijitokeza kwa kuwa hakuna tume huru ambayo ingesimamia uchaguzi bila ya kupendelea chama chochote.

Pia alisema Chadema imejipanga kushika dola na wana uhakika wa kushinda uchaguzi huo endapo serikali itakubali kuundwa tume huru ya uchaguzi.

"Chadema tunaamini tuna wafuasi na wanachama wengi wanayoiunga mkono. Endapo serikali ikiunda tume huru ya uchaguzi, tunatangaza mapema kushika dola," alisema.

"Tunadai tume huru kwa sababu tumekuwa wahanga (waathirika) wa uchaguzi mbalimbali kipindi cha nyuma na awamu hii hatutaki yatokee," aliongeza Kimambo.

Katika hatua nyingine, Kimambo alifungua milango kwa vijana wa Chadema kutumia fursa ya uchaguzi kugombea nyadhifa mbalimbali za uongozi ili kulikomboa taifa.

Mwenyekiti huyo alisema Bavicha wamekusudia kufanya ziara na mikutano ya hadhara katika majimbo saba ya uchaguzi Mkoa wa Arusha, lengo likiwa kuhamasisha vijana kushiriki na kugombea nafasi za ubunge na udiwani.

Aidha, alisema Bavicha imeanzisha utaratibu wa kufanya siasa za kidigitali kwa ajili ya kupashana habari. Alisema kila mwanachama wa Chadema atapaswa kuwa na simu janja itayomwezesha kupata taarifa za matukio mbalimbali ya chama kwenye mtandao.



# Wachangamkia uzalishaji fiwi

**Na Mwanahamisi Jingu,** MWANGA

KASI ya wananchi wa vijiji vya pembezoni katika Wilaya ya Mwanga, kuchangamkia kilimo cha uzalishaji wa fiwi kwa ajili ya malighafi ya viwandani, imeanza kutia moyo baada ya serikali kufungua milango.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusiana na maendeleo ya zao hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Zefrin Lubuva, alisema idadi ya wakulima waliojitokeza kulima zao hilo ambao linastahimili ukame kwa muda mrefu inatia moyo.

Halmashauri hiyo mpaka sasa, imetenga hekta 750 za ardhi ambayo inatoa fursa ya uwekezaji wa shughuli za kilimo.

"Tumekwenda kukagua mashamba darasa pamoja na wakulima wanaolima zao hilo na tumeridhishwa na idadi ya waliojitokeza kulima fiwi mwaka huu. Zao hili lina mafanikio makubwa kiuchumi na soko kubwa liko nchi za Kenya na India ambako wananchi wake wengi hupenda kutumia kama chakula," alieleza.

Fiwi ni aina fulani ya maharage jamii ya kunde, ambayo hulimwa katika maeneo yenye ukame, kwa sababu zao hilo hustahimili sana ukame kwa muda mrefu.

Aidha, alisema ardhi hiyo imetengwa katika Kata ya Kirya, Kileo na Kivulini. Katika Kata ya Kirya peke yake kuna jumla ya hekta 900 za umwagiliaji ambapo hadi sasa hekta 150 tu ndizo ambazo zinatumika.

"Wawekezaji wanakaribishwa kuja kuendeleza hekta zilizo baki ambazo zina rutuba nzuri na hali ya hewa nzuri inayoruhusu kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo hili. Eneo lingine ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni Kijiji cha Kileo chenye jumla ya hekta 2,400 ambazo zinafaa kulimwa kwa kipindi chote cha mwaka," amesisitiza mkurugenzi huyo.

Kijiji cha Kivulini chenyewe, kina jumla ya hekta 1,050 ambapo hekta zinazotumika kwa kilimo ni 400 tu.

Wakati katika Tarafa ya Jipe Ndea, nayo imetengwa kama maeneo yenye ardhi ya kutosha inayofaa kwa kilimo. Mazao yanayostawi ni alizeti, mtama, uwele, miwa, mahindi, maharage, ngwara, korosho, mbogamboga, matunda na mpunga.



Baadhi ya vifaa vya Chuo cha Uongozi wa Maendeleo Kilolo, vikiwa vimekusanywa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, jana, ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Asia Abdallah (hayupo pichani), baada ya kuviondoa, kwenye ghala la Kijiji cha Kitowo, ambalo lilikuwa linatumika kama chuo, kutokana na mmiliki wake kushindwa kulipa kodi ya pango.
**PICHA: MPIGA PICHA WET**

# Serikali yaelekeza nguvu shule msingi

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SERIKALI imesema kwa sasa inaelekeza nguvu kwa walimu wa shule za msingi za Wilaya ya Siha, kuanza kufundisha kwa mbinu za elimu jumuishi, miundombinu na njia bora zaidi za kujifunzia na kufundishia ili kuongeza fursa ya watoto wenye ulemavu wa akili, usonji na ulemavu mwingine.

Jana, Ofisa Elimu wa Elimu Maalum wa Wilaya ya Siha, Rashidi Mgonja, alisema kazi ya kwanza ni kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha shule za msingi, kubaini mahitaji maalum ya mwanafunzi katika ujifunzaji na ufundishaji.

Alikuwa akitoa mada kwa wadhibiti ubora wa elimu, maofisa elimu, waratibu wa elimu kata, walimu wakuu na walimu wa kawaida kutoka kata mbili za mfano za Karansi na Sanya Juu waliokuwa wakipigwa msasa kuhusu mradi wa kujenga uelewa wa pamoja juu ya utekelezaji wa elimu jumuishi unaotekelezwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Connects Autism Tanzania (CAT).

"Tunachotaka hapa ni kutoa afua stahiki kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi katika madarasa jumuishi. Elimu jumuishi ni njia ya ufundishaji inayolenga kuwasaidia na kuwahudumia wanafunzi wenye ulemavu katika muundo wa madarasa ya kawaida.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Daniel Lema, akifungua mafunzo hayo aliwataka wataalamu hao kuona ni jinsi gani kutatengeneza mikakati ya kufundisha kwa kutumia mbinu za elimu jumuishi zitakazowasaidia watoto bila kubagua wenye mahitaji maalum na wale wasio na mahitaji maalum.

"Tumepata upendeleo wa hali ya juu kwa kuwa tumepata mwarobaini wa tatizo hili na tunategemea tutakuwa pilot wa mkoa wa Kilimanjaro (sehemu ya mfano). Hii elimu au mafunzo haya yatatusaidia wilaya yetu kutoa elimu kwa wale wenye mahitaji maalum na wale wasiokuwa na mahitaji maalum katika shule zetu zote za Wilaya ya Siha.

Lema alisisitiza: "Walimu wetu wote watakuwa committed (wajibu wa lazima) kutoa hii elimu jumuishi kwa wanafunzi wote na niseme pia juhudi ambazo zimeonyeshwa na CAT (Connects Autism Tanzania) ni juhudi kubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania."

Kwa mujibu wa Lema, Wilaya ya Siha inao wanafunzi wengi wenye mahitaji maalum lakini ni mahali gani watakwenda kupata elimu yao, ndipo tatizo linapoanzia.

"Unakuta hilo la kuwa na mahali watoto hao wanapewa elimu hii, ndio tatizo na kuwatenga kwa maana ya kuwaweka katika shule maalum nayo inakuwa ni tatizo. Lakini kama watapata hii elimu jumuishi kwa maana ya wale wenye mahitaji na wasio na mahitaji itatusaidia sana kurahisisha malengo ya kuwapa elimu na wao," alieleza Lema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Connects Autism Tanzania, Graceanna Lyimo, alieleza kuwa kilichowasukuma kupeleka mradi huo kinatokana na dhamira yao njema ya kutaka kuona jinsi gani watashirikisha elimu huyo kwa watu wenye watoto wenye matatizo ya akili.

"Tulianza na Mkoa wa Arusha, lakini mikoa ya Kanda ya Kusini nao walishaanza, Mbeya na Iringa wako vizuri kabisa na tuna imani tutafika katika elimu jumuishi kama tutatambua elimu jumuishi ni haki na nchi yetu imesaini mkataba wa kimataifa," alisema Lyimo.

# Bakwata yaja kivingine huduma za afya

**Na Godfrey Mushi**, MOSHI

BARAZA Kuu la Waislamu mkoani Kilimanjaro (Bakwata), limetangaza nia yake ya kuanza kuwasaidia wagonjwa mbalimbali kufikia huduma za afya kwa kuwakatia bima, badala ya kuwapa fedha.

Hayo yamo katika taarifa ya katibu wa baraza hilo mkoani hapa, Awadhi Lema, aliyoitoa jana wakati wa uzinduzi wa bima ya afya kwa waumini wake.

"Bakwata Kilimanjaro tumesema wagonjwa wote wanaokwenda katika misikiti mbalimbali kwa ajili ya kuomba fedha ili wakapate matibabu, kwa sasa tutawakatia bima ya afya badala ya kuwapa fedha," alisema Lema.

Alisema Bakwata imepitisha mpango huo na kuanzia sasa itawakatia bima ya afya iliyoboreshwa (iCHF) wahitaji hao, badala ya kuwapa fedha, hasa kutokana na udanganyifu unaofanywa na wahitaji.

Lema alisema wagonjwa wengi wamekuwa wakifika katika misikiti mbalimbali ya mkoa huo kwa ajili ya kuomba msaada wa fedha ili wakapate matibabu hospitalini lakini hawafanyi kama walivyoomba fedha.

Kutokana na uamuzi huo, Bakwata imeonya waumini wake kuacha tabia ya kuwachangia fedha wahitaji hao kuanzia sasa na badala yake wawaelekeze kuna huduma hiyo.

"Kuanzia leo misikiti yote, akija mgonjwa anayeomba fedha kwa ajili ya matibabu akatiwe bima ya afya ambayo itamsaidia mwaka mzima. Bima tuliyopitisha iwasaidie wahitaji haizidi Sh. 30,000 na asipewe fedha mkononi," aliagiza Lema.

Kwa mujibu wa Lema, katika msikiti wa Riadha peke yake kwa siku moja wahitaji zaidi ya watano hujitokeza wakiomba fedha kwa ajili ya kwenda hospitali kupata matibabu.

Mmiliki na Mkurugenzi wa Kampuni ya usafirishaji wa abiria inayomiliki mabasi ya Ibra Line, Ibrahim Shayo, alijitolea kuwakatia bima ya afya Maimamu wa misikiti 36 wa Manispaa ya Moshi.

Ufadhili huo wa Ibra Line una thamani ya Sh. milioni 1.8.

Kwa upande wake, mratibu wa bima hiyo mkoa wa Kilimanjaro, Bogias Mwamgunda alisema kwa sasa bima hiyo mgonjwa atatibiwa kuanzia ngazi ya zahanati, kituo cha afya na hospitali ya mkoa.

"Kitaifa tuna lengo angalau la kuandikisha kufikia asilimia 30 kwa kaya zote kujiunga katika bima hii na katika mkoa wa Kilimanjaro tumefikia asilimia 21.3 na kimsingi kwa takwimu hiyo utaona bado tupo chini katika uandikishaji," alieleza Mwamgunda.



Ukurasa 20

Mdudu rushwa sasa atua kwa wakubwa wa dunia



Ukurasa 15

Bilionea Mzimbabwe amaliza mgomo wa madaktari kwao


# BUFE

Ijumaa Januari 24, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 18

## Ilivyokaa tafsiri benki, chimbuko lake na safari yake ilikofika nchini



# Mapambano ya Takukuru yanapofungua macho ugonjwa sugu wizi ndani ushirika

**Na Nimi Mweta**

KIASI cha Sh. bilioni nne na ushee za wakulima zilizoibwa na maofisa wa ngazi tofauti za vyama vya ushirika pamoja na vile vya kuweka na kukopa zimepatikana na zinarudishwa kwa wakulima, kwa mujibu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Hatua hiyo ni sehemu ya kazi za taasisi hiyo.

Alichosema Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali Joseph Mbungo, ni kuwa fedha hizo zimepatikana katika Vyama vya Ushirika vya Kuuza Mazao (AMCOS), vyama vya ushirika vya jumla na vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (SACCOS).

Ni baada ya ukaguzi maalum uliofanyika katika mikoa 28 Bara, licha ya kuwa kuanzia mwanzo hali ilikuwa tete zaidi mikoa ya kusini, kutokana na wizi mkubwa wa fedha za malipo ya korosho.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Pata somo la umaskini, tabia zake na namna ya kuukabili

Ukurasa 14

UCHUMI

# Pata somo la umaskini, tabia zake na namna ya kuukabili





Shughuli za uwajibikaji, kuufuta umaskini na kutafuta mafanikio ya kiuchumi katika picha tofauti.

**Na Mwandishi Wetu**

UMASKINI ni nini? Huo ni ukosefu wa mahitaji ya msingi ya binadamu kama vile chakula, maji salama, huduma za afya, mavazi na nyumba kutokana na kukosa uwezo wa kuvinunua. Pia, inajulikana kama umasikini uliokithiri au fukara.

Ni kadri kuwa na rasilimali chache zaidi au mapato madogo zaidi kulingana na watu wengine katika jamii au nchi au hali ya wastani duniani. Hali hiyo pia inajulikana kama umaskini halisi au unyonge.

Hali hiyo ni hali ya kuwa na rasilimali chache au kipato cha chini kuliko wengine kwenye jamii au nchi, au ikilinganishwa na wastani duniani kote.Umaskini unajumlisha, pia matokeo yake upande wa siasa na jamii.

Kupunguza ufukara ni kati ya malengo makuu ya taasisi nyingi za kimataifa, kama vile Umoja wa Mataifa na Benki ya Dunia, inayokadiria watu milioni 702.1 waliishi kifukara mwaka 2015 na ilopofika mwaka 1990, walikuwa bilioni 1.75, kati yao milioni 347.1 walikuwa Afrika Kusini kwa Sahara.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (Unicef), inakadiria nusu ya watoto duniani wanaishi kifukara.

**ASILI YAKE**

Asili ya umaskini inatajwa ni kiwango cha chini cha utajiri na uzalishaji, pia mfumuko wa bei wa bidhaa duniani; vikwazo kwa uzalishaji; kukosekana nia ya serikali na wenye mamlaka kuwajali wa chini.

> **Kuwapo afya duni na ukosefu wa elimu nafuu kunaathiri uzalishaji chakula cha kutosha na kinachoipatia umma mlo sahihi na unaotakiwa.**



Inaacha maswali katika kufikia safari ya mafanikio kiuchumi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Kuwapo afya duni na ukosefu wa elimu nafuu kunaathiri uzalishaji chakula cha kutosha na kinachoipatia umma mlo sahihi na unaotakiwa.

Katika mataifa yanayoendelea, inakadiriwa asilimia 40 ya watoto wenye umri wa miaka minne kwenda chini wana ugonjwa wa anaemia utokanao na kukosa madini ya chuma.

Vilevile ulevi wa pombe na dawa ya kulevya, unaweza kuwaweka watu katika umaskini unaoendelea, ikongezwa na maradhi ya kuambukizwa kama vile malaria na kifua kikuu, yote yanasababisha umaskini kwa umma.

Hiyo ni kwa sababu ya kutumika rasilimali za kifedha, ambazo zingetumika katika uwekezaji na uzalishaji. Lingine ni vita, migogoro ya kisiasa na uhalifu, inayojumuisha vikundi haramu vinavyozua vurugu na vikundi vya walanguzi wa dawa ya kulevya pia vinaweka vikwazo kwa uwekezaji.

Kuna ripoti, vita vya wenyewe na migogoro Afrika vimeligharimu dola bilioni 300 kati ya mwaka 1990 na 2005 na kiwango cha



umaskini kinaongezeka.

Vipengele vya utamaduni, kama vile ubaguzi wa aina mbalimbali, nao unatajwa kuathiri uzalishaji.

Upungufu wa mahitaji ya msingi Kupanda kwa gharama ya maisha, kunawafanya umaskini kuzidi, bajeti za watu maskini kutumika kununua chakula zaidi, ikilinganishwa na wenye nacho.

**HAIBA YA MASKINI**

Kuna tabia kadhaa zinazoelezwa na watafiti kumtawala masikini. Moja, anajenga tabia ya muda mwingi anajikita kuangalia televisheni, sinema na tamthiliya, badala ya kufanya shughuli za kuingiza kipato au hata shughuli za ziada zenye manufaa fulani.

Pili, ni ununuzi wa chakula zilizoandaliwa kama chipsi pizza na 'baga': Hiyo ni tabia nyingine inayotajwa kumsukuma mtu katika umaskini, ikiwa dalili mbaya inayohitaji marekebisho ya haraka.

Hivyo vyakula vyenye mafuta mengi na kusababisha magonjwa kama uzito uliopitiliza na moyo. Yote yanampunguzia mtu ufanisi wa kazi, hata kuwa na madhara katika uchumi, akili, kijamii na hata uhusiano binafsi na ina matumizi makubwa ya pesa yanayoepukika.

Tatu, kuchelewa kuamka: Ni tabia inayojitokeza kwa kijana, ni ishara ya kuukaribisha umasikini katika siku za usoni. Vijana wanakuwa wazembe kufanya kazi kwa bidii na kwa vile hawatumii umri wao vizuri, wanakuwa hawajawekeza kwa baadaye.

> **“ Upungufu wa mahitaji ya msingi kupanda kwa gharama ya maisha, kunawafanya umaskini kuzidi, bajeti za watu maskini kutumika kununua chakula zaidi, ikilinganishwa na wenye nacho.**

Inaelezwa hata matajiri duniani kama Bill Gates, Elon Musk, Mark Zuckerberg wana tabia ya kuamka mapema kuanza kufanya kazi zao kwa bidii kila siku

Nne, kulaumu wengine kwa unayopitia: Wataalamu wa uchumi wanaeleza moja ya tabia zinazomfanya mtu awe maskini, ni kulaumu wengine kwa kutofanikiwa kwako na kusahau usemi “Maisha ni jinsi unavyoamua kuyaona.'

Tano, kutoweka akiba ambayo kimsingi ni jambo la msingi sana katika mapato yoyote yanayopatikana, kusaidia pindi likitokea matatizo ya baadaye, kama dharura ya ugonjwa.

Sita, inahusu ununuzi wenye mpangilio: Wataalamu wanashauri kufanya ununuzi ukiwa tayari umeandika orodha ya vitu unavyotaka na siyo kukurupuka bila ya mpangilio. Pia, kama unachukua mkopo, itafakariwe kwa ajili ya nini wenye manufaa gani.

Saba, inagusa uzazi wa mpango: Mtu anatakiwa kuhakikisha hali yako ya uchumi iko imara kabla haujaanza kuzaa watoto hao na inaelezea kitaalamu, watoto wakiwa wengi kwenye familia kuliko uwezo binafsi, umasikini unakuwa jirani kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kuwahudumia kwa wakati.

Saba, inaangukia suala la upimaji afya kila mara: Inawezekana kwa wengi linaonekana sio la msingi kupima afya kila mara, lakini ni la msingi kwa kuwezesha kuishi ukiwa na uhakika wa afya yako, ikiwa ni njia nyeupe kuelekea mafanikio.

Ni kama ilivyo mfano kwa ugonjwa wa saratani unavyohimizwa kwamba, suala la kujua mapema hali ilivyo kiafya, ndio uhakika wa kutibiwa na kupona mapema

Nane, inahusu matumizi ya pesa kabla ya kupata: Tabia ya kukopa pesa kabla hazijapatikana kwa matarajio ya kuzilipa pindi zitakapopatikana, ni dalili ya ama umaskini kunyemelea au kuukaribisha mwenyewe.

Wataalamu wanashauri kufanya kazi kwanza na kupata pesa kisha uendelee na kufanya matumizi unayonuia.

Tisa, kunahitajika kuwa na marafiki wasio na malengo makubwa: Marafiki wanakusaidia kufikia malengo yako uliyojiwekea, pia wana nafasi ya kufanya usifikie malengo. Hivyo, inashauriwa kutumia muda zaidi na marafiki wenye malengo makubwa kimaisha, wanawaza mambo chanya na sio mambo hasi muda wote.

Hilo linasaidia kutunza muda, kutokata tamaa kwenye malengo yako au kuwa mbunifu zaidi, hata kukukosoa kwa tabia zinazorudisha nyumba maendeleo yako.

*• **Kwa mujibu za taarifa mawasilisho ya kitafiti na uchumi.***

# Bilionea Mzimbabwe amalizamgomo wa madaktari kwao



Madaktari wa Zimbabwe walipoandamana. **PICHA: MTANDAO**

MADAKTARI nchini hapa wamekubali kurejea kazini, kwa kumaliza mgomo uliodumu kwa zaidi ya miezi minne.

Mgomo huo unaingia katika rekodi iliyodumu kwa muda mrefu zaidi katika historia ya nchi hiyo na umeathiri vibaya mno sekta ya afya Zimbabwe.

Madaktari hao wamekubali kurejea kazini baada ya bilionea raia Zimbabwe anayeishi Uingereza, Strive Masiyiwa, kufikia makubaliano nao kuwa kuwa atamlipa kila mmoja wao marupurupu ya takriban dola za Zimbabwe kwa mwezi za usafiri kwenda kazini, kupitia mfuko wa hazina utakaoanzishwa kushughulikia hilo.

Madktari wengi waliokuwa katika mgomo, wanapata mshahara chini ya dola 100 kwa mwezi. Bilionea huyo atagharamia mahitaji hayo ya madaktari kwa miezi sita. Haijabainika wazi ni kipi kitafuata baada ya kipindi hicho.

Ni mgomo ulioanza mwezi Septemba mwaka jana, baada ya kushindwa kufikia makubaliano na serikali ya Zimbabwe, madaktari zaidi ya 200 walifukuzwa kazi kwa kosa la kufanya mgomo.

Madaktari waliofutwa kazi, walikutwa na hatia ya kutokuwapo kazini, bila ya likizo wala sababu muhimu' kwa siku tano zaidi kwa mujibu wa taarifa ya Bodi ya Huduma za Afya (HSB)

Madaktari hao wamekuwa wakidai malipo mazuri ya mishahara na ni mgomo uliosababisha kuzorota huduma katika hospitali kubwa, ambazo huduma za dharura pekee ndizo zimekuwa zikitolewa.

Msemaji wa Chama cha Madaktari nchini humo, Dk. Tawanda Zvakada, anasema ni miezi mitano anaingia hospitali bila kutoa huduma.

“ Nilipoingia kwenye wodi ya hospitali kwa mara ya kwanza, nilikuwa na hisia mchanganyiko. Nimefurahi kurejea, lakini hakukuwa na vifaa vya kutosha kwetu sisi kutoa huduma bora”, amesema Zvakada.

Kwa mujibu wa Dk. Zvakada, hali ilikuwa ya kuridhisha kwa sababu madaktari wamerejea, wodi zimefunguliwa na sehemu za kuona madaktari zilizofungwa, sasa zimefunguliwa tena.

Madaktari wanasema kwamba, walitaka suluhu ya kudumu lakini hawakuweza kufikia makubaliano na serikali na kurudi kwao sasa kumetokana na makubaliano na asasi inayoongozwa na tajiri huyo.

“Watu wamepoteza maisha, wengine wamepata ulemavu ambao hauwezi kurekebishika,” anasema Dk. Zvakada.

Aidha, madaktari hao wanaeleza matumaini kwamba watafikia makubaliano ya kudumu na serikali, wakitoa na wito wa kuangaliwa kwa madai yao ambayo hayajabadilika. **BBC**

BIASHARA

# Mapambano ya Takukuru yanapofungua macho ugonjwa sugu wizi ndani ushirika

## • Imefukua mabilioni njia panda ya kuondolewa



Mkuu wa mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, akizungumza na viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi Wilaya ya Mkuranga. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**INATOKA UK.13**

Wakati serikali inajitahidi wananchi wafaidike, wajanja ushirika wanafaidi kwanza, na kama hatua maalum hazikuchukuliwa, hesabu zao za kila mwaka zingepitishwa tu kero zitolewe majibu ya haraka na kadhalika.

Cha kushangaza, ni kuwa ukaguzi wa hesabu za vyama mbalimbali vya ushirika unafanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Ushirika (COASCO), ambalo lilieleza katika taarifa ya awali kuwa kulikuwa na ubadhirifu au wizi mkubwa wa fedha.

Hilo halishangazi kusikia. Kwa upande mmoja COASCO ni mkaguzi wa nje kwa kila chama cha ushirika au aina ya ushirika kwa jumla, lakini wakati huohuo kuna aina ya 'nidhamu ya kijumuia' kuwa wao pia ni wanaushirika, hivyo suala la kulindana linakuwa tata.

Ndiyo sababu ya kuhitajika mkaguzi halisi wa nje, Takukuru; amri ambazo inatii au inazielewa ni tofauti na za COASCO.

Ilibidi Waziri wa Kilimo Japhet Hasunga aiombe Takukuru kuingilia katika suala hilo, baada ya COASCO kutoa taarifa inayoonyesha kuwa ubadhirifu mkubwa ulionekana katika uendeshaji wa vyama vingi vya ushirika.

> “Hapa vinaangaliwa vitu vingi, eneo linapokuwa bandari hiyo bubu, mazingira kama ni salama au si salama, na zile ambazo zitakuwa na sifa zitarasimishwa na kuingizwa kwenye mfu-

Mtu anaaweza kusema kuwa hata COASCO waliona mazingira yamebadilika, hivyo ikabidi wawe wakweli kwa kiwango kinachostahili kwani ingekuwepo sababu ya kuhisi kuwa wameshiriki huo 'mchezo mchafu' wa uendeshaji vyama vya ushirika, kwa kuwafichia madudu ya hesabu zao, ingekuwa tatizo kwa viongozi wake wa juu.

Hiyo ndiyo hasa athari ya 'kutumbua majipu,' operesheni ya awali ya kurudisha nidhamu serikalini na kutojua nani atakayesema iwapo madudu yapo.

Licha ya kiwango hicho cha fedha kilichookolewa, ambacho hata katika mazingira ya sasa kingetosha kuridhisha watu kuwa kazi imefanyika kupambana na wizi na ubadhirifu, TAKUKURU inasema bado inaendelea na kazi.



Mkutano wa wana ushirika Liwale.

### MAKUNDI YA UKAGUZI

Yako mafungu mawili ya fedha yanayoingia katika ukaguzi, moja ni Sh. bilioni 51 ambayo tayari limefanyiwa ukaguzi wa kina, na eneo lingine lina jumla ya Sh. bilioni 7, na ukaguzi wake unaendelea.

Hakuna kusimamisha ukaguzi njiani, kuwa hapo tulipofika tayari panaridhisha, tungoje sasa mwaka mwingine.

Jumla ya vikundi 4413 vya ushirika vimekaguliwa vikiwAmo vyama 38l vya ushirika, vyama 2710 vya ununuzi wa mazao, vyama 1448 vya kuweka na kukopa na mashirika au vikundi vingine 217 ambako jumla ya Sh. bilioni 124 zilipitia kwa vikundi hivyo, na zilionyesha ukakasi katika maeneo mengi.

Kuna mazingira mapana zaidi ya tatizo hilo kwani uendeshaji wa vyama vya ushirika una walakini, hata kwa ngazi ya usajili wake, uwepo wake kwa maana ya mikutano ya kila wakati, uchaguzi wa viongozi na kutunza hesabu za vikundi hivyo.

Hiyo si kwa mujibu wa Takukuru, ila mkaguzi wa ndani COASCO, ambaye taarifa yake ya mwaka jana ilisema kulikuwapo vyama 11,410 vya ushirika vilivyosajiliwa na kati ya hivyo, vyama 6,463 angalau vinafanya kazi, vingine 2,844 vimedorora na vyama takriban 2,103 vilikuwa havionekani yaani ukifuatilia hukuti kitu, vimepauka au kuyeyuka.

Ina maana, ilifikia mahali watu wakaacha kuja katika mikutano au wakasahau walikuwa wanadai nini au wamechangia nini, wakauza mazao kwa wafanyabiashara, mambo yakaisha. Ipi sababu?

Kama ilivyotazamiwa maeneo ya Pwani ambako korosho inalimwa kwa wingi ndiyo yaliyoongoza katika tuhuma za ubadhirifu ambazo Takukuru imeainisha, kwa mfano mkoa wa Lindi unaongoza kwa ubadhirifu unaoainishwa wa shilingi zaidi kidogo ya bilioni moja.

Pia, uko Mkoa wa Njombe uliofikia kiwango kama hicho cha shaka ya wazi ya ubadhirifu unaofikia Sh. bilioni moja, wizi wa ngazi ya kutisha.

Mkoa wa Mtwara ulifuata kwa mbali tuhuma za Sh. milioni 681.2, na wabadhirifu wanaofuata wana nusu ya kiwango hicho, kwa mfano Songwe ilifikia tuhuma za ubadhirifu wa Sh. milioni 354.3l na Pwami tuhuma za ubadhirifu unaofikia Sh. milioni 291.4.

Kuna mikoa mingine miwili iliyofikia tuhuma za wizi zaidi ya Sh. milioni 100, ambayo ni Mara, wenye tuhuma za wizi wa Sh. milioni 242.9 na Iringa, kwa tuhuma za wizi unaofikia Sh. milioni 133.8 kwa mauzo tofauti kulingana na mazingira.

Iko mikoa inayodhaniwa kufikia makumi kadhaa ya mamilioni ya wizi, na mingine kadhaa hata haikufikia tuhuma za wizi zinazofikia milioni 10, kwa mfano Mkoa wa Arusha ambako tuhuma dhidi yake zilifikia Sh. milioni 1.2 tu.

Ukiangalia hesabu hizo, unakuwa alichosema Rais Dk. John Magufuli kuhusu wakulima wa korosho kuibiwa takriban Sh. bilioni 1.2 na vyama vya ushirika kimedhihirishwa na kuzidi.


Ukichukua Mkoa wa Lindi pekee, unapata karibu hesabu yote hiyo wakati bado fedha nyingi zinatuhumiwa kuibwa Mkoa wa Mtwara na hata Pwani.

Na kwa upande mwingine, juhudi hizi zimeambatana na serikali kuingilia kati kuhusu bei ya korosho kwani kuwapo kwa fedha nyingi zaidi kwa ajili ya wakulima kunaweza pia kuchochea wabadhirifu, kuwa 'leo ni leo, asemaye kesho mwongo.' Mvua hiyo ya mawe huenda isinyeshe tena na kama mtu hatakuwa amefaidi hapo itakuwa ndiyo basi tena kwake.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru, Brigedia Jenerali John Julius Mbungo.

# Biashara katika picha




Mkurungenzi wa Biashara wa kiwanda ya kuzalisha saruji cha Mbeya, Mark Chilambe (kulia), akikabidhi kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (wa pili kulia), mfano wa hundi ya Sh. milioni 300, ikiwa ni gawio la serikali, katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma jana. Wa pili kushoto ni Naibu Waziri wa Fedha, Dk. Ashatu Kijaji, Msajili wa Hazina, Athuman Mbutuka. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Wachuuzi wa mahindi mabichi wakiyamenya maganda kabla ya kuyauza katika soko la Mawasiliano, Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Dada mchuuzi wa miwa akisaka wateja katika eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

UCHUMI

# Ilivyokaa tafsiri benki, chim lake na safari yake ilikofika




Jengo kongwe na benki ya NBC, jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

MTU anaweza kuhoji benki ni nini? Inaangukia katika tafsiri ni taasisi ya kifedha iliyopewa jukumu kuu la kuweka amana za fedha za watu na kutoa mikopo kwa wateja wake na inalipa riba kwa amana.

Pia, benki ina jukumu la kutoa ushauri wa kifedha na miradi, pale kunakohitajika.

Majukumu mengine ni huduma za usimamizi wa mali, ubadilishaji fedha kama za kigeni na kuna aina kuu za benki; biashara, kijamii kama ushirika vijijini na uwekezaji

Hata hivyo, kwa hatua zilizopigwa hivi sasa, kuna benki za mtandaoni na za imani za kidini, zikizingatia taratibu za jamii wateja wake kupata huduma za kibenki.

Majukumu makuu ya benki za biashara ni kutoa mikopo ya muda mfupi, kutoa na kuweka amana za wateja mbalimbali wenye akaunti.

Benki za rasilimali zenyewe zinaenda mbali zaidi ya mkopo na uwekaji amana, kusaidia maandiko mbalimbali ya kibiashara, katika kufanikisha matumizi ya mkopo wanayoitaka.

Lakini, benki zinawajibika na kusimamia kiwango cha fedha za kimataifa sokoni, kudhibiti mfumuko wa bei na kiwango cha pesa kilichopo katika mzunguko.

> **"Hadi sasa benki kuu zilizoko katika orodha ya kuwa na mtaji mkubwa duniani ni za nchi za Marekani, Uingereza, Japan, Uswisi, na China.**

Hata hivyo, aina ya benki kitaifa unategemea sera na malengo ya nchi na hali ya soko la sekta hiyo katika wakati husika, mathalan Tanzania katika zama za Sera ya Ujamaa na Kujitegemea.

Hadi sasa benki kuu zilizoko katika orodha ya kuwa na mtaji mkubwa duniani ni za nchi za Marekani, Uingereza, Japan, Uswisi, na China.

Katika hatua za awali za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) yenye umri zaidi ua miaka 50 sasa, majukumu yake makuu yanayomuisha benki zingine nchini, utoaji wa sarafu na noti, kushauri serikali kuhusu masuala la fedha na mkopeshaji.

**DEREVA WA UCHUMI**

Benki ni moja wa madereva muhimu wa uchumi kitaifa, kupitia utoaji ukwasi unaohitajika kwa familia na biashara kuwekeza na sasa kuna benki zinazotoa huduma za mtandaoni, akiba na mikopo zinategemea rehani zilizopo.

Benki za biashara, kimsingi zinazingatia biashara, pia zinatoa huduma zaidi na wateja binafsi na kujenga uhusiano nao. Hata hivyo, ni utendaji unaosimamiwa na benki kuu inayosimamia mengi, ikiwamo mitaji yao na sera za uendeshaji wake.



Jengo Benki ya Tar nia (Bo jijini D Salaar

**NCHINI TANZANIA**

Historia ya milki za benki nchini inaanzia mwaka 1965 ya kupitishwa kisheria na kutekelezwa mwaka 1966. Hapo ndipo kukashuhudiwa kuundwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Ni katika kipindi nchini ikatawaliwa katika mfumo wa uchumi wa kijamaa.

Sura nyingine ni zao la kutanuka benki kupitia utekelezaji wa Azimio la Arusha mwaka 1967 na kuzaliwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ambayo ikawa na matawi mengi nchi nzima.

Ni benki ambayo ilipewa jukumu kubwa la kusukuma mageuzi katika utekelezaji wa Mpango wa

# buko nchini





la Kuu nza- oT), Dar es n.



Wateja wa benki wakiwa katika foleni ya huduma.

Kwanza wa Maendeleo ya Uchumi wa Miaka Mitano (1964-1969) katika kutafuta upatikanaji huduma za msingi.

Ilikuwa wakati kunaundwa viwanda vipya vya kuzalisha mahitaji ya kila siku kwa lengo la 'kutumia tunavyozalisha' na si 'kutumia tusivyozalisha.' Ni zama iliyojengwa viwanda vingi sana nchini.

Ilipofika awamu ya pili ya utekekelezaji Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ( 1969 - 1974), ilikuwa ni mwendelezo wa mpango uliopita, ulioshuhudia maboresho zaidi, ikiwamo katika sekta ya viwanda.

Ni awamu iliyoanzishwa benki maalum za kuboresha mahitaji ya mkakati ya kisekta ya serikali. Itakumbukwa, Benki ya Nyumba Tanzania (THB), yenyewe ilibuniwa kuboreskha mkakati wa kiserikali ulioanza tangu baada ya uhuru.

Mfano mmojawapo ni mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba, kupitia kuwakopesha wananchi mwaka 1966, na wanapitia taratibu, mfano hai jijini Dar es Salaam, katika maeneo kama Kinondoni, Mwananyamala, Magomeni, Temeke na Ilala.

Ni zama kulikoanziswa shirika la Msajili wa Majumba, ambalo ni zao la Azimio la Arusha, sambamba na kuwapo Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Wananchi walijengewa nyumba

> **"Hapo kukawapo hata mapitio ya majukumu ya BoT katika kusimamia benki kitaifa. Hadi kufikia mwanzoni mwa miaka ya 1990 kulishuhudiwa sheria mpya za fedha na kibenki kitaifa.**

mbalimbali kwa mikopo nafuu serikalini na hivyo katika mipango ya maendeleo ya baadaye ikawa ni zaidi ya miaka 10 ya uhuru, THB ikatanua wigo wa jukumu hilo kwa kuendeleza sekta ya ujenzi, ikiwa kwa mwezeshaji muhimu.

Aidha, sekta ya kilimo na mifugo, ikaundiwa Benki ya Ushirika na Mendeleo Vijijini (CRDB), ambayo ilifanywa mwezeshaji maalum katika eneo hilo muhimu la kiuchumi na mwajiri mkuu wa kitaifa, kukibatizwa "uti wa mgongo wa taifa,"

Katika hatua nyingine, mipango mikubwa ya serikali kama vile ya kuinua viwanda vikubwa kitaifa, ukiwamo uliopangwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa Viwanda na uendelezaji wa huduma za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (Sido) kwa tija zaidi ziliundwa muwezeshaji ambaye ni Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB).

## BAADA MAGEUZI

Mageuzi ya kiuchumi duniani ya mwaka 1985, yana historia kubwa katika mageuzi ya sekta ya kifedha nchini, zikiwamo benki.

Hapo kukawapo hata mapitio ya majukumu ya BoT katika kusimamia benki kitaifa. Hadi kufikia mwanzoni mwa miaka ya 1990 kulishuhudiwa sheria mpya za fedha na kibenki kitaifa.

Ni wakati kulikoanza kushuhudiwa soko huria la fedha za kigeni, jambo ambalo awali lilikuwa jukumu maalum la BoT, tena ziliuzwa kwa kibali malaum.

Ndani ya muda mfupi maduka ya fedha za kigeni ambayo yametoweka katika siku za karibuni, yalitapakaa katika sehemu nyingi za nchini, sambamba na uuzwaji huo katika benki, hapo ikajenga maana ya benki mbalimbali kuanzisha vitengo vya kusimamia uzaji fedha za kigeni.

Wakati huo, pia serikali ilikuwa inafanya mageuzi makubwa kupitia iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma(PSRC), kwa kubinafissha taasisi za umma.

Sekta ya Benki haikubaki salama, kwani iliyokuwa benki ya THB ilifikia hatua kutoweka sokoni, kutokana hali yake kiuchumi kulegea mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Hata baadhi ya mitaji ya kigeni haikuwa salama, kwani kuna benki ya Greenland mwishoni mwa miaka ya 1990, ililazimika kufungwa ndani ya saa 24 na BoT, ambayo ina mamlaka kwa mujibu wa sheria.

NBC ambayo ilikuwa benki kubwa zaidi nchini, ilivunjwa kuzalisha taasisi tatu, ikiwamo NBC (1997) Limited na National Microfinance Bank (NMB), ambayo ilibaki na sehemu ya asilimia ya miliki ya serikali.

Aidha, CRDB ilibinafishwa na hisa zake kuingia katika mikono ya miliki binafsi na katika mbinu ya kibiashara kutopoteza nembo ya soko la asili, NBC na CRDB hazikubadili sana majina yao kwa kiasi kikubwa.

NBC na CRDB katika majina yao mapya, yaliondokana na ufafanuzi wa kirefu cha majina yao ya awali.

Pia, ni mageuzi yaliyofika mbali kwa mageuzi ya baadhi ya majukumu maalum kuachwa na zote kuwa katika mwonekano zaidi kujikitia katika maisha mapya sura ya benki ya biashara.

Vivyo hivyo, mchakato wa kubinafsishwa benki hizo, uliendana na kuweka kando baadhi ya majukumu ambayo si ya asili kibenki kama vile kumiliki majengo.

TIB ndio haikuguswa na mageuzi hayo, ila baada ya kulega kwa muda mrefu, serikali ilipatia mtaji mkubwa katika njia ya kuchangia kuinua mitaji, rasilimali na uwekezaji kitaifa.

Ni mageuzi ambayo Benki ya Posta, iliyoanzia kitengo katika Shirika la Posta Tanzania (TPB), nayo ilipata uhai kamili kama shirika la umma, katika hadhi ya kibenki inayoendelea kukua.

Baada ya miaka nenda rudi, Benki ya Maendeleo ya Kilimo nayo imeundwa nchini, ambayo pengo lake liliachwa na CRDB iliyokuwapo kabla ya ubinafsishaji.

Mageuzi ya hivi karibuni ya kijinsia, yalisukuma kuundwa Benki ya Wanawake, ambayo katika tathmini kiataifa, ilihamishiwa kuwa sehemu ya benki nyingine, aina ya msukosko uliyoikuta benki ya Twiga.

Baada ya mageuzi ya kibenki nchini, ndipo kumeshuhudiwa utitiri wa taasisi hizo zikianzishwa kila mahali, kutoka mitaji ya nchini na ya kigeni ikiwamo, za jumuiya ya kijamii.

Kimsingi, BoT ambayo zaidi ya miaka 50 ilikuwa na majukumu makuu sita, hivi sasa yameongezeka maradufu kulingana na mahitaji na mageuzi yanayoendelea nchini na duniani.

Mojawapo ya majuku yake ni hatua yake ya karibuni iliyochukua kufungia maduka ya fedha za kigeni kutokana na ilichokiona kuwapo ukiukaji wa maslahi ya umma.

## JUKUMU LA BOT

Kwa mujibu wa tovuti yake, jukumu la msingi la Benki Kuu ya Tanzania, ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kudhibiti mfumuko wa bei na kujenga mfumo wa fedha ulio imara na unaofaa kwa ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa.

Kazi Zingine: Kutoa sarafu ya nchi ambayo ni Shilingi ya Tanzania.

• Kusimamia mabenki na taasisi za fedha

• Kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini

• Kuhifadhi akiba ya nchi ikiwamo fedha za kigeni

• Kutoa ushauri juu ya masuala ya uchumi na fedha kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

• Benki ya Serikali, na

• Benki ya Mabenki.

UCHUMI

UTAFITI TRANSPARENCY:

# Mdudu rushwa sasa atua kwa wakubwa wa dunia

• Denmark, New Zealand juu, kwenye vita Afrika mkiani



Sudan Kusini, ambako athari za vita zimeiingiza katika rekodi mbaya ya rushwa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MATAIFA yenye nguvu za kiuchumi duniani sasa yanatazamwa jicho la kipekee, kutokana na kuguswa katika madai ya kuhusika na vitendo vya rushwa.

Ripoti ya hivi karibuni ya shirika la Transparency International, imezitaja nchi zinazoongoza katika vitendo vya kifisadi katika ngazi za kibiashara ni pamoja na Canada, Ufaransa, Uingereza na Marekani.

Inaeleza nchi hizo ni vinara katika ushawishi wataalamu na wakurugenzi wa kibiashara. Mkuu wa Transparency International, Delia Ferreira Rubio, anasema hatua ya kuguswa na vitendo vya rushwa kwa serikali za nchi hizo, inatokana na ukosefu wa imani katika taasisi na umuhimu wa uadilifu wa kisiasa.

Ndani ya ripoti kuna orodha ya nchi na kanda kulingana na mitazamo ya viwango vya ufisadi katika serikali zao, kwenye kipimo wanachokitaja 'kuanzia 0 hadi 100.'

Namba 'sifuri' huashiria sekta ya umma ambayo ina rushwa zaidi. Jumla ya nchi 180 hushirikishwa na matokeo hutegemea tafiti za wataalamu na wakurugenzi wa kibiashara.

> **Nchi zinazofuata ni Finland, Singapore, Sweden, Uswisi, Norway, Uholanzi, Kanada, Luxembourg, Ujerumani na Uingereza zinashikilia nafasi 10 za juu.**

Nchi za Denmark na New Zealand zimepata pointi nyingi katika kupambana na rushwa, huku Somalia, Sudan Kusini na Syria zikishika mkia.

Matokeo mabaya ya mataifa wanachama wa kundi la G-7 yanayoongoza uchumi wa dunia, yameonyesha hali ya kutopiga hatua mbele katika vita dhidi ya rushwa.

Canada ilishuka nafasi nne nyuma ikilinganishwa na mwaka wa 2018. Ufaransa na Uingereza zilishuka daraja kwa pointi, huku Marekani ikishuka chini kwa pointi mbili.

Aidha, Ujerumani na Japan hazikusajili mabadiliko yoyote, lakini Italia ilipiga hatua moja mbele na utafiti huo umebaini kuwa nchi ambako vyama vya kisiasa vinafadhili uchaguzi, ziko katika hatari ya kushawishiwa na makundi yenye malengo maalum ya kimaslahi na hazina uwezo wa kukabiliana na ufisadi.

Rubio anasema, ni lazima serikali ishughulikie suala la fedha kutumika kwa njia ya ufisadi ili kushawishi na kutoa shinikizo katika mifumo ya siasa.

Marekani imeorodheshwa nafasi ya 69 mwaka huu, hiyo ikiwa mbaya zaidi iliyowahi kushika katika kipindi cha miaka minane iliyopita.

Nchi 22 zilisajili mabadiliko makubwa katika vita dhidi ya rushwa kati ya mwaka 2012 na 2019, nyingine ni Ugiriki, Guyana na Estonia.

Nchi 21 zilisajili matokeo mabaya katika orodha hiyo ikiwa ni pamoja na Canada, Nicaragua na Australia.

Denmark na New Zealand ndizo zilishika nafasi ya kwanza bora, zikiwa na pointi 87 huku Somalia, Sudan Kusini na Syria zikiorodheshwa katika nafasi za mwisho.

Shirika la Transparency International, linasema kushindwa kwa jumla katika kudhibiti rushwa kunachangia mgogoro wa demokrasia na uchumi duniani kote.

Kwa kuzingatia maeneo ya kikanda nchi za Ulaya ya Magharibi na hasa Umoja wa Ulaya, ndizo zimepata wastani wa alama 66.

Ukanda unaoshika mkia ni nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, zikiwa na wastani wa alama 33.

**AFRIKA JE?**

Ripoti hiyo inasema Afrika limeshindwa kutafsiri ahadi zake za kupambana na rushwa katika maendeleo halisi na nchi zinazokabiliwa na vita kama vile, Somalia, Syria na Sudan Kusini zina viwango vya juu vya ufisadi.

Mkurugenzi wa Transparency International, Patricia Moreira, anasema juhudi zaidi zinahitajika kuimarisha ukaguzi na uwajibikaji kwa ajili ya kulinda haki za raia na uchumi endelevu.

**HALI IKOJE?**

Denmark na New Zealand zimeendelea kuongoza kuwa nchi zenye vitendo vichache vya rushwa katika miaka ya hivi karibuni na ziliongoza pia mwaka uliopita.

Nchi zinazofuata ni Finland, Singapore, Sweden, Uswisi, Norway, Uholanzi, Kanada, Luxembourg, Ujerumani na Uingereza zinashikilia nafasi 10 za juu.

Ni mara ya kwanza Marekani kutoingia kwenye nchi 20 zisizokuwa na hali mbaya ya ufisadi tangu mwaka 2011.

Nchi za Asia ya Ukaneda wa Pacific, zina jumla ya alama 44, wakati Ulaya ya Mashariki, Asia ya Kati zikiwa na wastani wa alama 35 na Marekani zina wastani wa alama 44.

China imepata wastani wa alama 39 na hivyo kushika nafasi ya 87 nyuma ya India iliyo katika nafasi ya 78 kwa kupata wastani wa alama 41. Russia iko kwenye nafasi ya 138.

** Kwa mujibu wa taarifa za DW na vyombo mbalimbali.*



## HABARI MBEYA



Moja ya magari ya kubeba taka katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, likiwa limefunga barabara ya City Garden, wakati lilipokuwa linashusha ghuba tupu na kubeba lililojaa takataka kwa ajili ya kusafirisha kupeleka katika dampo kuu, lililopo katika eneo la Nsalaga, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Fedha zakwamisha ujenzi wa shule

**Na Nebart Msokwa,**
BUSEKELO

UKOSEFU wa Sh. milioni 300 umekwamisha ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Busokelo wilayani Rungwe, mkoani Mbeya ambayo inalenga kupokea wanafunzi wa vipaji maalumu kutoka katika halmashauri hiyo.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Busokelo, Forkward Mchami, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa iliyokuwa na lengo la kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa.

Alisema halmashauri hiyo kwa sasa haina fedha za kukamilisha ujenzi wa shule hiyo, hivyo wanategemea kuwatumia wadau mbalimbali wa maendeleo ili wawasaidie kuikamilisha na ifunguliwe Januari, mwakani.

Mchami alisema shule hiyo ni muhimu kwa maelezo kuwa ikishakamilika na kufunguliwa, itasaidia kukabiliana na upungufu wa vyumba vya madarasa kama ambavyo tatizo hilo linasumbua halmashauri nyingi.

"Pia hii shule tuliamua kuijenga kwa sababu watoto wengi wanaofaulu mitihani ya darasa la saba na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika halmashauri hii, wanakuwa na sifa za kwenda shule za vipaji maalumu lakini shule za aina hiyo ni chache," alisema Mchami.

Aliwaomba viongozi wa CCM kuisaidia halmashauri hiyo kuwahamasisha wadau mbalimbali ili washiriki ujenzi huo na shule ikamilike mapema.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Anania Lawrence, alisema shule hiyo awali ilikuwa inajengwa kwa nguvu za wananchi, lakini baadaye wakaikabidhi halmashauri ili iendeleze baada ya wao kushindwa.

Alisema shule hiyo haiwezi kukamilika kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri kwa kuwa ni madogo na wakitegemea mgawo kutoka kwenye mapato hayo, haitamalizika mapema.

Lawrence alisema katika mwaka wa fedha wa 2019/20, halmashauri ilitenga Sh. milioni 50 pekee kwa ajili ya mradi huo, hivyo wanahitaji nguvu zaidi ili kuendeleza ujenzi huo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Solomoni Itunda, alisema walibaini kuwa ina tatizo la mapato duni hali ambayo inalazimu miradi mingi kutegemea fedha kutoka serikali kuu. Alisema baada ya kubaini tatizo hilo, wameamua kulichukua suala la ujenzi wa shule hiyo ya wavulana kwa ajili ya kuliweka kwenye mikakati yao ya kusaidia miradi.

Alisema halmashauri hiyo ina miradi mingi ya maendeleo ikiwamo ya maji ambayo inagharimu fedha nyingi, lakini michango ya halmashauri ni kiasi kidogo.

"Halmashauri hii inakusanya Sh. milioni 400 pekee kwa mwaka, lakini ina miradi mingi. Sisi chama tunaona hii shule hawataweza kuikamilisha, hivyo tunalichukua kwa ajili ya kwenda kulifanyia kazi," alisema Itunda.

# Mgogoro wananchi, wawekezaji wafikia tamati

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imemaliza mgogoro wa kugombea eneo la kuchimba madini katika Kijiji cha Sangambi kati ya wananchi wa kijiji hicho na wawekezaji.

Kutokana na kumalizika kwa mgogoro huo, serikali imewataka wananchi wawe na utamaduni wa kufuata sheria.

Mgogoro huo uliibuka mwaka 2016 baada ya Wizara ya Madini kuwakabidhi leseni ya uchimbaji wawekezaji wawili, Singu Duwila na Staford Mwanzyala kwenye eneo lililokuwa limetengwa na kijiji kwa ajili ya msitu.

Inadaiwa kuwa wawekezaji hao baada ya kukabidhiwa eneo hilo, walifanya mazungumzo na viongozi wa kijiji na kukubaliana kuwa watakilipa kijiji Sh. milioni 15 na wakalipa Sh. milioni 13 tu.

Ofisa Madini Mkazi wa Wilaya ya Chunya, Godson Kamihanda, alisema leseni waliyopewa wawekezaji hao ni halali kwa mujibu wa sheria, hivyo walitakiwa waendelee na kazi baada ya kukubaliana na kijiji.

Alisema mgogoro uliibuka baada ya baadhi ya wananchi wa kijiji hicho kuanza kudai kuwa fedha ambazo wawekezaji hao walilipa ni kidogo, hivyo wakawa wanataka waachiwe waendelee kuchimba wenyewe.

Alisema wawekezaji hao waliamua kutulia kwanza na kuacha kuliendeleza eneo hilo na wakaanza kufuata taratibu za kisheria ili waendelee kuchimba.

"Tatizo ni kwamba wananchi hawajui sheria za madini. Haya madini kwa mujibu wa sheria ni mali ya Watanzania wote lakini inaonyesha hapa wananchi walikuwa wanataka kujimilikisha, hivyo ni vyema tukakaa mezani na kuelimishana ili shughuli ziendelee," alisema Kamihanda.

Diwani wa Sangambi, Njunjulu Mhewa, alisema mgogoro huo haukuwa na afya, hivyo ni vyema serikali kuingilia kati ili kuumaliza na eneo liendelezwe.

Alisema kama inawezekana ni vizuri wananchi wakawaachia wawekezaji waliendeleze au wawekezaji warudishiwe fedha zao ili kijiji kifuate taratibu upya ya kuchukua leseni mpya kutoka Wizara ya Madini.

Akionyesha ramani ya kijiji hicho ambayo inaonyesha eneo hilo la Mtafla kuwa liliachwa na kijiji kama eneo tengefu baada ya wakati wa kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, Mhewa alisema yeye hafungamani na upande wowote.

"Migogoro ya aina hii sio mizuri kwa sababu inakwamisha maendeleo, sasa ni vizuri serikali ifanye uamuzi sahihi ambayo hautaumiza upande wowote kati ya hizi zinazolumbana. Wawekezaji wana leseni na naamini fedha zao zingesaidia hata maendeleo ya kijiji na kata," alisema Mhewa.

Mkuu wa Wilaya, Maryprisca Mahundi, aliwaonya wananchi kuacha kutoa uamuzi kwa mihemko kwa maelezo kuwa kufanya hivyo kunazorotesha maendeleo yao wenyewe. Aliwataka wawekezaji hao ambao ni wazawa, kulipa fedha zilizobaki ili waendelee na kazi huku akiwataka wananchi kuwapa muda wawekezaji kutafuta fedha hizo kwa maelezo kuwa kwa muda wote tangu walipopata leseni walikuwa hawazalishi.

Aliutaka uongozi wa kijiji cha Sangambi kwa kushirikiana na Ofisi ya Madini ya Wilaya, washirikiane kuandaa orodha ya watu wote wenye leseni ya kuchimba madini katika msitu huo ili wachangie shughuli za maendeleo.

"Kwa taarifa nilizo nazo ni kwamba msitu huo una zaidi ya wachimbaji 200 wenye leseni, hivyo tunatakiwa tuwe na takwimu sahihi. Kwa sasa nawaomba wananchi jitahidini kufuata sheria ili migogoro ya aina hii isijirudie," alisema Mahundi.

# Wahofia kufukuzwa kwenye mashamba

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WAKAZI wa Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wanaotumia mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na Kiwanda cha Tanganyika Parkers kwa ajili ya kilimo, wameanza kupata wasiwasi wa kuporwa maeneo hayo baada ya serikali kuanza mipango ya kujenga chuo kikuu.

Mashamba hayo yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 6,000 yamekuwa yakitumiwa na wananchi kutokana na Kiwanda hicho cha Tanganyika Parkers kutofanya kazi tangu kilipojengwa miaka ya 1970.

Hivi karibuni, serikali ilitangaza kutaka kutumia sehemu ya mashamba hayo kwa ajili ya ujenzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na kiwanda cha dawa.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wananchi hao wanaolima mashamba hayo walisema wanayategemea kwa ajili ya kuzalisha chakula na ikitokea wakazuiliwa itakuwa tatizo kubwa kwao.

Mmoja wa wakulima hao, John Mwasile, alisema mashamba hayo wanayategemea kwa ajili ya kulisha mji wa Mbalizi kutokana na mazao mengi kulimwa huko.

Alisema binafsi analima ekari 12 ambazo zote zimo ndani ya eneo ambalo serikali inakusudia kujenga chuo, hivyo itakuwa tatizo kubwa kwake pamoja na familia yake.

"Hatuwezi kupinga maendeleo na tutapisha ili chuo hicho kijengwe lakini tutapata shida ya kupata mashamba mbadala ya kuzalisha chakula," alisema Mwasile.

Hivi karibuni, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Jakaya Kikwete, alitembelea eneo hilo na kutangaza kuwa muda wowote ujenzi wa tawi la chuo hicho utaanza.



# Asilimia 80 ya pamba yauzwa nje

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema asilimia 80 ya pamba imeuzwa nje ya nchi katika msimu uliopita.

Aidha, ameagiza kampuni 23 ambazo zilinunua pamba kwa wakulima kuwasilisha taarifa za mauzo kabla ya Januari 31, mwaka huu.

Bashe alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano baina ya wanunuzi wa pamba, wauzaji pembejeo na taasisi za kifedha uliofanyika jijini hapa.

Alieleza kuwa kampuni hizo zilinunua pamba tani 350,000 msimu huo chini ya usimamizi wa serikali. "Baada ya taarifa hizi kuwasilishwa tutakutana pamoja kwa lengo la kujadili utekelezaji wa uuzaji ulivyokuwa, ili kujipanga kwa ajili ya msimu ujao, lengo ni kujua jinsi soko lilivyokuwa," alisema.

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema kuwa msimu ujao wa mavuno ya pamba malipo yote yatafanyika kupitia benki na si kulipana mkononi.

"Kuna tatizo sasa hivi wanunuzi wanadaiwa fedha za Amcos, wanadaiwa fedha za kodi kutoka halmashauri, na kipaumbele ilikuwa ni kuwalipa wakulima, lakini Amcos zimetumia fedha za malipo ya wakulima kwa ajili ya shughuli za uendeshaji kwa hiyo unakuta baadhi ya wakulima wachache wanadai fedha zao," alisema Bashe.

"Unakuta mkulima aliuza pamba ya Sh. milioni 1.2 halafu kalipwa Sh. milioni 1.1 bado Sh.100,000 hajalipwa na Amcos yake, kwa hiyo tunafanya kazi ya kukusanya takwimu hizo kupitia bodi, taarifa hiyo inatakiwa kupatikana kabla ya Januari 31, 2020 ili kuifanyika kazi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Benki, Abdumajid Nsekela, alisema kazi hiyo imefanywa kwa ushirikiano na wizara, taasisi za fedha na wanunuzi wa pamba.

"Tumeunda kikosi kazi kidogo kikijumuisha benki, wanunuzi wa pamba, wizara husika pamoja na Benki Kuu ili kukusanya takwimu sahihi kwa lengo la kuziangalia kwa pamoja na kuzifanyia maamuzi," alisema Nsekela.



Baadhi ya wajumbe wa kikao cha Baraza Kuu la Chama cha Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania (TRAWU), wakishiriki kuimba wimbo wa mshikamano wakati wa ufunguzi wa kikao cha baraza, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima wataka wataalamu kukabili magonjwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeombwa kupeleka wataalamu vijijini kwa ajili ya kutoa elimu ya matumizi ya dawa za kutibu wadudu wanaoharibu zao la zabibu kutokana na wakulima kutokuwa na uelewa huo.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi wa kikundi cha Mbukwenyi, Evarist Maganga alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kero wanazokutana nazo katika kilimo hicho. Alisema wakulima hawana elimu ya utunzaji zabibu pale zinapokumbwa na magonjwa wanashindwa kujua watumie dawa gani.

"Ni muhimu elimu ya utumiaji dawa ifike vijijini ili kunusuru zabibu isipate magonjwa wengi hawajui wanapata hasara," alisema Maganga.

Naye mkulima Emanuel Chibada, alisema skimu ya umwagiliaji wa zao la zabibu ni nzuri lakini tatizo ni utunzaji ili kukabiliana na wadudu waharibu. Alisema wakulima wengi wanahitaji somo kuhusu kilimo hicho kwa kuwa zao hilo ni muhimu katika kuwainua wananchi kiuchumi.

"Tunaomba wataalamu wa kilimo wapite maeneo ya vijijini kutusaidia kutupa mafunzo wakulima wa zabibu itasaidia kwa kiasi kikubwa kuinua wakulima wa zao hili hapa nchini," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa kikundi cha Mbukwenyi, Julius Sombe, alisema baada ya kuungana imekuwa rahisi kwao kupata mbegu bora pamoja na mbolea. Alisema pia wamenufaika na mkopo wa Sh. milioni 104 kutoka Benki ya NMB ili kuinua kilimo chao.

# Wafanyakazi reli watakiwa kujikita ulinzi miundombinu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAFANYAKAZI wa Kampuni za Reli Tanzania (TRC) na Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (Tazara), wametakiwa kuwashughulikia watu wanaohujumu miundombinu ya reli kwa kuwa wanasababisha hasara kwa serikali.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Reli nchini (TRAWU), Exervery Marko, wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa Baraza kuu la Wafanyakazi wa shirika hilo jijini hapa.

Alisema hivi karibuni baadhi ya wamebainika kutaka kuhujumu miundombinu ya reli, jambo ambalo linapaswa kulindwa na wafanyakazi hao ili serikali isiingie kwenye hasara hiyo.

"Nawaambia wajumbe wenzangu hawa watu ni maadui zetu namba moja maana wanataka kutia mchanga kitumbua chetu, tusikubali," alisema.

Aidha, alieleza kuwa serikali imewekeza fedha nyingi katika kuboresha miundombinu ya reli katika maeneo mengi nchini hivyo ni jukumu la wafanyakazi kuunga mkono juhudi hizo kwa kuilinda.

"Kazi ya chama chetu ni kutetea na kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi wote hivyo ni haki ya wanachama kuhakikisha wanafanyakazi ili kufanikisha malengo ya shirika," alisema.

Aliwataka wafanyakazi hao kuwa wazalendo kwa kufanyakazi kwa kuzingatia maadili ya kazi na kuepuke malalamiko yasiyo na msingi.

Aliishukuru serikali kwa kuwekeza fedha nyingi kwenye shirika hilo ambayo kwa sasa linahudumia kwa ufanisi ndani na nje ya nchi.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Trawu wanawake Taifa, Theresia Mahagatila, aliiomba serikali kuendelea kutoa nafasi za kazi na kuongeza vyeo mahali pa kazi bila upendeleo.

"Mfumo dume bado haujaisha katika maeneo ya kazi, hivyo ni jukumu letu kinamama tuliopo kwenye nafasi za uongozi kushirikiana ili kuonyesha ufanisi katika kazi," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa Trawu Taifa, Shehe Shuguli, alisema kwenye baraza hilo wamepitisha rasmi uongozi wa juu wa baraza hilo baada ya uliokuwapo kuondolewa rasmi kwa tuhuma za kukiuka masharti ya uongozi wao.



# Watoto 11 walawitiana, sheha alaumu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATOTO 11 wa kiume wenye umri usiozidi miaka 12 katika Shehia ya Mchikichini Wilaya ya Magharib 'A' Unguja wanadaiwa kulawitiana wenyewe kwa wenyewe.

Kutokana na tukio hilo, imemlazimu sheha wa shehia hiyo kuwaita watoto hao na kujua chanzo chake.

Akizungumza na Nipashe, Sheha wa Shehia hiyo, Kijakazi Feruz Khamis, alisema awali alipata taarifa ya watoto wawili wa kiume wamelawitiana baada ya kuwahoji kwa undani watoto hao.

Alisema baada ya mahojiano, watoto hao waliwataja wenzao tisa ambao hufanya nao kitendo hicho.

"Nasikitika sana baadhi ya wazazi wa watoto hawa baada ya kupata taarifa zao niliwaita na kuwaeleza hali ilivyo, lakini baadhi yao hawajaonyesha ushirikiano," alisema Khamis.

Khamis alisema kati ya watoto hao 11 amegundua kuwa mtoto mmoja ndiye aliyewafundisha watoto wenzake 10 kutokana na mtoto huyo kuharibiwa na kaka yake ambaye alikuwa akiishi naye nyumba moja.

"Mtoto mwenyewe ameeleza kuwa kaka yake aliyekuwa akiishi naye nyumba moja ndiye aliyeanza kumlawiti, lakini kaka huyo baada ya kusafiri ndipo akawa anawatafuta watoto wenzake ili kumfanyia kitendo hicho," alisema Khamis.

Khamis alisema kaka wa mtoto huyo ambaye alikuea akiishi naye ndiye aliyeanza kumfanyia kitendo hicho na kumtishia asitoe taarifa vinginevyo atamuua.

Mama mlezi watoto hao ambaye hakutaka jina lake kuandikwa, alisema ameshtushwa kupata taarifa hizo, lakini anashangazwa kuona baba mzazi wa mtoto huyo hana huduma yoyote kwa mtoto huyo wala kutoa ushirikiano dhidi ya kitendo alichofanyiwa.

"Huyu mtoto mimi ni mtoto wangu wa kambo namlea tokea mdogo alipotelekezwa na mama yake mzazi akiwa na umri wa miaka miwili na huyu mtoto wala hajui kuwa mimi si mama yake niliyemzaa," alisema mama huyo.

Alieleza kuwa licha ya kutelekezwa na mama yake akiwa na umri wa miaka miwili, hadi sasa anaumri wa miaka 11, lakini pia hivi sasa ametelekezwa na baba yake.

"Mume wangu ambaye ndiye baba mzazi wa mtoto huyu ametutelekeza... huu mwaka mmoja hana huduma yoyote anayoitoa, anaishi Tanzania Bara, huku tukiwa tunapata taabu chakula tunapewa na majirani," alisema mama huyo.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Magharibi 'A', Sabra Ali, alisema amepokea taarifa ya watoto hao na kusema kuwa chanzo cha kuongezeka kwa vitendo hivyo ni baadhi ya wazazi kukimbia majukumu yao ya kutoa huduma hasa kinababa kuwaachia malezi kinamama.

# Balozi Seif Iddi sasa azitaka kampuni kusaidia wenye uhitaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema utayari wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC) wa kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu ni jambo jema na linalopaswa kuendelea kuungwa mkono na taasisi nyingine.

Balozi Iddi aliyasema hayo jana ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar wakati wa mazungumzo na uongozi wa kampuni ya TCC ambao upo Zanzibar kwa ajili ya kutoa msaada wa vifaa kwa watu wenye ulemavu.

Alisema zipo taasisi na kampuni nyingi ndani na nje ya nchi zenye uwezo na fursa kubwa ya kusaidia kundi hilo maalumu, lakini mengi yamekuwa hayawasaidia jamii zenye uhitaji.

Balozi Iddi aliushukuru na kuupongeza uongozi huo kwa uamuzi na moyo wake wa kizalendo wa kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum kwa kuwasaidia vifaa pamoja na uwezeshaji wa kiuchumi.

"Serikali ya Zanzibar inathamini jitihada za kampuni ya TCC na itajitahidi kuunga mkono katika kuona changamoto zinazoikwaza kampuni hiyo katika harakati zao za kusaidia jamii zinaondoka," alisema Balozi Iddi.

Naye Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa kampuni hiyo, Godson Kiliza, alisema uamuzi wa kampuni hiyo wa kuanzisha mradi wa kusaidia kundi la watu wenye mahitaji maalumu ni kurejesha fadhila kwa jamii.

Alisema mradi huo ulioanza kwa takriban mwaka mmoja sasa kwa kushirikiana na serikali kupitia Shirikisho la Jumuiya ya Walemavu nchini, umekuwa ukiwapatia vifaa tofauti watu wenye mahitaji maalumu.

Alisema vifaa hivyo ni pamoja na baiskeli za watu wenye mahitaji maalumu, magodoro na fimbo hutolewa sambamba na kuwapatia baadhi ya watu wenye mahitaji maalumu duka kwa lengo la kuendesha biashara ndogo ili kukidhi mahitaji yao ya msingi.

Kiliza alisema baadhi ya watu wenye mahitaji maalumu wa Mikoa ya Tanga, Pwani, Dodoma, Geita na Temeke jijini Dar es Salaam wameanza kufaidika kupitia mradi huo.

Alieleza bajeti ya mradi huo kwa mwaka 2019 ambayo ni endelevu inamalizia katika visiwa vya Zanzibar na kwamba watu wenye mahitaji maalumu wapatao 210 kutoka Unguja na Pemba wanatarajiwa kunufaika.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kulia), akizungumza na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC), Godson Kiliza (wa pili kushoto), na ujumbe wake mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yawapatia vitendea kazi maofisa kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imedhamiria kuwapatia wafanyakazi wa mkoa huo vifaa vya kufanyia kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na ufanisi zaidi.

Aliyasema hayo juzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja wakati akiwakabidhi vyombo vya usafiri ikiwamo pikipiki 16 na gari moja la kubebea wagonjwa maofisa kilimo na misitu wa wilaya hiyo.

Alisema lengo la kutolewa vifaa hivyo kwa wafanyakazi ni kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya kuwahudumia wananchi hasa wakulima wa Wilaya ya Kati bila ya kupata vikwazo vya aina yoyote.

Aliwataka wafanyakazi waliokabidhiwa vyombo hivyo kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa kwenda kwa wananchi kuwasikiliza na kuwasaidia katika kutatua changamoto zinazowakabili katika harakati zao za maisha.

Vilevile aliwataka wafanyakazi hao kuhakikisha wanavitunza vyombo hivyo ili viweze kudumu kwa muda mrefu kwa sababu vimenunuliwa kwa gharama kubwa.

"Natoa onyo kwa yeyote atakayeshiriki katika uvujishaji mapato atashughulikiwa, wala hatoonewa haya, kwani katika jambo hilo sina mzaha wala sitomwonea mtu huruma," alisema Mahmoud na kuongeza:

"Nawaasa madaktari wenye tabia ya kuwatolea wagonjwa lugha zisizofaa wanapofika kwenye vituo wajirekebishe mara moja wapeni moyo wagonjwa ili wapate faraja na muwape matibabu mazuri," alisisitiza Mahamoud.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, alisema lengo la kutolewa vyombo vya usafiri kwa wafanyakazi ni kuwawekea mazingira mazuri ya kutekeleza majukumu waliopewa ya kuwahudumia wananchi kwa wakati mwafaka.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kati, Said Mtaji Askari, alisema kupatiwa vyombo vya usafiri wafanyakazi ni kutekeleza azma ya serikali ya kuimarisha sekta za afya, kilimo na elimu.

# Mabula akwazwa maofisa ardhi kufanywa kama watoto wa kambo

**Na Munir Shemweta,**
UVINZA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,. Angeline Mabula, ameijia juu Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma kwa kushindwa kuihudumia Idara ya Ardhi na kusababisha watumishi kujigharamia baadhi ya vifaa ili kutekeleza majukumu yao.

Hali hiyo ilibainika juzi katika halmashauri hiyo wakati Naibu Waziri akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika mkoa wa Kigoma.

Akiwa katika masjala ya ardhi ya halmashauri hiyo, Mabula alibaini utunzaji majalada ya ardhi usiofuata taratibu huku baadhi ya hati zikiwa hazijakamilishwa ili kuwapatia wamiliki wa ardhi tangu mwaka 2018.

Kutokana na hali hiyo, aliwajia juu watumishi wa sekta ya ardhi katika halmashauri kwa kushindwa kutekeleza majukumu ipasavyo, jambo alilolieleza kuwa linachangia uwapo wa migogoro ya ardhi sambamba na kuwanyima wananchi fursa ya kupata hati.

Mabula aliagiza hati zote ambazo taratibu zake zishakamilishwa ikiwamo wamiliki wake kutia saini kupelekwa Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Magharibi ndani ya wiki moja kwa ajili ya kukamilishwa na kupatiwa waombaji. Baada ya kuwajia juu watumishi wa ardhi katika halmashauri hiyo, ndipo Ofisa Ardhi wa Halmashauri, anyama Makongo, alipomweleza kuwa idara hiyo inashindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na kukosa vifaa jambo lililosababisha kuamua kuchukua 'printer' yake binafsi na kuipeleka ofisini kwa ajili ya kusaidia kazi za idara.

Hali hiyo si tu ilimshutua na kumshangaza Naibu Waziri bali ilimsononesha kwa kuona watumishi wa sekta hiyo katika halmashauri wanatumia fedha zao za mifukoni kuendesha ofisi jambo alilolieleza kuwa halikubaliki.

'Hapa jitihada za ziada zinahitajika, halmashauri ipo inashindwa kuihudumia idara ya ardhi halafu watumishi wanatumia fedha zao za mfukoni? Hili halikubaliki lazima niwasiliane na Waziri (Selemani) Jafo kuhusiana na suala hili," alisema.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mabula, idara za ardhi katika halmashauri nyingi nchini zimekuwa kama watoto wa kambo kutokana na wakurugenzi wa halmashauri kutozitengea bajeti ya kutosha jambo linalofanya idara kufanya kazi katika mazingira magumu.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, Lillian Matinga, na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Enelia Lutungulu, wamewaokoa maofisa ardhi wa halmashauri hiyo wasitumbuliwe kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo ikiwamo kutokamilisha utoaji wa hati za ardhi kwa muda mrefu.

Walionusurika ni Ofisa Ardhi Mteule, Spear Mwalukasa ambaye ilielezwa yuko katika mafunzo na Ofisa Ardhi Ezekiel Bichuro.

Hata hivyo, Matinga na Lutungulu waliwatetea kwa kueleza kuwa hawana muda mrefu katika idara hiyo na makosa yanaweza kuwa yalifanywa na maofisa waliopita.



Baadhi ya vijana wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mkoa wa Iringa, wakisaidiana na mafundi kusomba mawe kwa ajili ya ujezi wa makazi ya Katibu wa UVCCM wa mkoa huo, James Mgego (mwenye kofia ya pama), wakati wa zoezi la kuchimba msingi wa nyumba hiyo, juzi. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Zabuni huduma viwanja vya ndege kutangazwa

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku nane kumalizika kwa mkataba wa kutoa huduma kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), imesema itatangaza zabuni mpya kwa watu kuanza kupeleka maombi yao.

Baadhi ya wadau wa sekta hiyo walionyesha wasiwasi wao kutokana na kuchelewa kutangazwa kwa zabuni hiyo kutokana na mkataba wa anayetoa huduma kwa sasa kutarajiwa kwisha Januari 31, mwaka huu.

Wadau hao wamekuwa na wasiwasi na kuzitaka Mamlaka za TAA na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), kuhakikisha uwazi na usawa katika zabuni za kutoa huduma katika uwanja huo ambao una watoa huduma watatu.

Mkataba huo hutolewa kwa miaka mitano kwa anayeshinda zabuni hiyo, na huduma zinazotolewa ni kushusha na kupakiza mizigo, kuhudumia abiria, ngazi za kupandia na kushuka kwenye ndege.

Kampuni zinazotoa huduma hizo ni Swissport Tanzania ambaye mkataba wa haki ya kutoa huduma unakwisha Januari 31, mwaka huu, na kampuni nyingine ni Nas-Dar Airco.

Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Julius Ndyamukama, alisema wanatarajia kutangaza zabuni za kazi hiyo mwezi ujao.

"Tunatarajia kufungua zabuni kwa kila anayeona anasifa za kutoa huduma hizo aombe, mchakato utakuwa wazi kabisa na kila mmoja anakaribishwa," alisema.

Aidha, idadi ya watoa huduma inayotakiwa kwa kwa mujibu wa TCAA ni KIA (2), Mtwara (1), Dodoma (1), Songwe (1), Mwanza (1) na watatu JNIA.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Swissport Tanzania, Mrisho Yassin, alisema kampuni yake inasubiri kutangazwa kwa zabuni hiyo na watashindania kwa kuwa wamekuwa wakitoa huduma kwa muda mrefu.

"Tunazisubiri mamlaka zitangaze zabuni hiyo nasi tutawania kwa kuwa tumekuwa kwenye huduma hii kwa muda mrefu kwenye viwanja vya ndege kwa zaidi ya miaka 34," alisema.

# DTB- Tanzania yaja na mpango mkakati wa biashara 2020

**Na Mwandishi Wetu**

DIAMOND Trust Bank Tanzania Limited (DTB-Tanzania), imetangaza mpango mkakati wa biashara kwa mwaka 2020 ikidhamiria kuongeza idadi ya wateja pamoja na kuongeza idadi ya matawi nchini.

Haya yaliazimiwa katika kikao cha 12 cha biashara kilichofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Katika kikao hicho ambacho hufanyika kila mwanzo wa mwaka kilipitisha kauli mbio ya mwaka 2020 "Mteja ni Kipaumbele Kwetu".

Akizungumza na waandishi wa habari katika kikao hicho kilichofanyika Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa DTB-Tanzania, Viju Cherian, alisema:

"Changamoto kubwa tuliyonayo kwa sasa ni namna ya kupata biashara ambayo itaendana na uwekezaji tuliyofanya katika nyanja za teknolojia. Agenda yetu ya kwanza mwaka huu ni kutoa kipaumbele kwa wateja wetu katika mikakati yote ya benki na kuongeza idadi ya wateja ndani ya benki. Ili kulifanikisha lengo hii, tumedhamiria kuboresha huduma kwa wateja hadi kufikia kiwango cha juu inayokubalika popote duniani.

Alisema wameandaa kalenda ya kuwanoa wafanyakazi wake wote wanaotoa huduma kwa wateja ili kuhudhuria mafunzo kwa vitendo katika kuwasiliana na kuwahudumia wateja wa aina zote mwaka huu. Benki imedhamiria kuboresha huduma zake sambamba na kuboresha viwango vya baishara na kuongeza matawi yake nchini.

Alisema benki hiyo imedhamiria kuongeza matawi mapya ambayo yanatazamiwa kuwa chachu katika kufikisha huduma za kifedha kwa Watanzania waliopo nje ya mfumo wa kibenki yakisaidiwa na njia mbadala ya huduma za fedha kama vile ATM, simu za mkononi na POS.

Benki ilifungua tawi jipya katika Manispaa ya Singida Desemba mwaka jana na pia imepanga kufungua tawi la pili katika visiwa vya Unguja-Zanzibar Aprili mwaka huu.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Rasilimaliwatu wa DTB- Tanzania, Makoye Ngofillo, alisema: "Wafanyakazi wenye hamasa na ueledi katika kuwahudumia wateja ndio watakaohitajika katika karne hii ya 21. Ni muhimu sana kuwashirikisha wafanyakazi katika maboresho ya huduma kwa wateja kwa njia ya mafunzo mbalimbali ndani na nje ya benki.

"Wafanyakazi wetu walioshiriki katika mkutano huu wa biashara wametoa mawazo chanya yatakayotumika kuunda mpango kazi wa upanuaji wa matawi ya benki na kuboresha huduma kwa wateja. Ni matumaini yangu kuwa kwa kupitia mafunzo mbalimbali, wafanyakazi wetu wapatao 550 watatoa huduma katika viwango bora zaidi."

DTB-Tanzania ni mshirika wa mtandao wa maendeleo ya kiuchumi wa Aga Khan Fund for Economic Development (AKFED) na pia ni sehemu ya mtandao wa benki za DTB Group zenye matawi zaidi ya 130 Afrika Mashariki katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Burundi.

## Wanajeshi wa FARDC wauawa

**KINSHASA,** DRC

WANAJESHI wawili wa serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wameuawa na kambi yao kuchomwa moto baada ya kushambuliwa na waasi wa FDLR katika eneo la Kakondo, wilayani Rutshuru, mashariki mwa nchi hiyo.

Viongozi wa serikali katika Jimbo la Kivu Kaskazini kutoka Wilaya ya Rutshukuru wamewashtumu waasi wa FDLR kwa kutekeleza mauaji hayo kwa kuwapiga risasi wanajeshi hao.

Elie Nzaani bunge wa eneo hilo alisema mbali na watu hao, wanajeshi wengi walitekwa katika kijiji cha Katwiguru na kuongeza kuwa, mauaji yameendelea kuzua hali ya wasiwasi.

Kwa upande wao watetezi wa haki za binadamu wamewataka waasi wilayani Rutshuru pamoja viongozi wa serikali jimboni Kivu Kaskazini kukaa kwenye meza moja kwa lengo la kudumisha amani na usalama wilayani humo.

Mwanaharakati Dunia Taabu amehuzunishwa kuona watu wanaendelea kuuawa wengi wakiwa ni raia wa kawaida.

Haya yanajiri wakati wananchi wamekuwa wakionyesha kuwa na imani na jeshi la nchi hiyo, huku wakiitaka serikali, kuongeza idadi ya askari wa kuulinda usalama wao kwenye maeneo yanayoshuhudia mapigano ya mara kwa mara.

Hadi sasa ni zaidi ya raia 10 ndio walioripotiwa kuuliwa kikatili na waasi hao wanaodaiwa kuwa wa FDLR tangu mwanzo wa juma lililopita. **RFI**

## Mtoto wa rais ashtakiwa kwa ulaghai

**LUANDA,** Angola

MTOTO wa aliyekuwa Rais wa Angola, Isabel dos Santos amefunguliwa mashtaka ya ulaghai baada ya kutuhumiwa kupora mali za taifa hilo.

Isabela ambaye ni mwanamke tajiri zaidi Afrika amefunguliwa mashtaka hayo na waendesha mashtaka wa Angola.

Mwanasheria Mkuu wa Angola, Helder Pitta Groz alisema kwamba madai hayo yanahusiana na wakati alipokuwa mwenyekiti wa kampuni ya mafuta ya Sonangol.

Groz alisema kwamba kibali cha kimataifa cha kuwakamata iwapo watakosa kujiwasilisha mbele ya mamlaka ya Angola kimeshatolewa.

"Isabel dos Santos anatuhumiwa kwa usimamizi na ufujaji wa fedha wakati alipokuwa mwenyekiti wa kampuni hiyo ya Sonangol hivyo basi amefungliwa mashtaka ya usimamizi mbaya wa ofisi, kutumia ushawishi wake na kughushi stakabadhi miongoni mwa uhalifu mwingine wa kiuchumi," alisema Gross. **BBC**

# Nkurunziza kulipwa mabilioni akiondoka madarakani

**BUJUMBULA,** Burundi

RAIS wa Burundi, Pierre Nkurunziza atapewa hadhi ya kuwa kiongozi mkuu wa nchi hiyo atakapoondoka madarakani.

Bunge la Burundi limepiga kura muswada wa sheria wa kumpatia Bwana Nkurunziza cheo cha "Kiongozi Mkuu" na kumpatia faranga za Burundi ($530,000) wakati atakapoondoka madarakani.

Burundi inajiandaa kwa uchaguzi mkuu Mei, mwaka huu na kwamba Nkurunziza aliahidi kuwa hatagombea tena muhula mwingine wa urais.

Muswada huo wa sheria pia utamwezesha kulipwa mshahara katika kipindi chote cha maisha yake, kupata marupurupu yote anayopewa makamu wa rais aliyeko mamlakani na atapewa nyumba ya kifahari, anayopewa kila Rais wa Burundi aliyechaguliwa kidemokrasia.

**Wabunge pia walipendekeza Rais Nkurunziza anapaswa kupewa cheo cha Kiongozi Mkuu na Bingwa wa Uzalendo.**

Ni Rais Melchior Ndadaye, aliyeuawa mwaka 1993, na Pierre Nkurunziza wenye vigezo vya kupewa marupurupu hayo.

Wabunge hao jana walifanya kikao juu ya kiwango atakachopewa rais anayeondoka madarakani, huku baadhi wakisema apewe milioni 500, huku wengine wakisema apewe faranga bilioni moja na wengine wakisema apewe faranga bilioni mbili.

Hata hivyo, baadaye walikubaliana apewe faranga bilioni moja na marupurupu mengine.

Wabunge pia walipendekeza Rais Nkurunziza anapaswa kupewa cheo cha Kiongozi Mkuu na Bingwa wa Uzalendo.

Pendekezo hilo lilipitishwa na kikao cha baraza la mawaziri katika jimbo la kisiasa la Gitega nchini Burundi.

Wananchi wa Burundi walijibu kwa hisia tofauti kuhusu muswada huo kwenye mitandao ya kijamii juu ya marupurupu yatakayotolewa Rais Nkurunziza; huku baadhi wakisema marupurupu ni mengi sana kwa nchi kama Burundi ambayo ni maskini duniani.

Wengine walisema kuwa kiasi hicho kinafaa kwa mtu anayelitumikia taifa mwenye majukumu ya hali ya juu. **BBC**



Askari wa Jeshi la Burundi akiwa amebeba silaha akipambana na wananchi baada ya kutokea vurugu. **PICHA: REUTERS**

# Kenya yachukua tahadhari kuhusu virusi

**NAIROBI,** Kenya

WIZARA ya Afya Kenya imeimarisha uangalizi katika bandari zake zote za kuingia na kuwapima raia wa kigeni wanaoingia kuona kama wana virusi vya corona.

Virusi hivyo hadi sasa vimeshaua watu 9 nchini China na takribani 400 wana maambukizi. Kenya imekuwa ikipokea wageni wengi kutoka China.

Kenya ni moja kati ya nchi iliyo hatarini kukumbwa na virusi vya Corona kutokana na mahusiano ya kibiashara na China.

Kila wiki, Shirika la Ndege la Kenya hupeleka ndege zake mbili katika Jiji la Guangzhou.

Mamlaka za China zimewataka watu kutosafiri ndani na nje ya mji wa Wuhan, mji ambao virusi hivyo vilipoanzia kisha kusambaa katika majimbo kadhaa ya China, pia nchini Marekani, Thailand na Korea Kusini.

Shirika la Afya Duniani (WHO) bado inafanya uchunguzi kufahamu kama mlipuko huo unaweza kuwekwa kwenye kundi la dharura ya kiafya kimataifa.

Hivi karibuni maofisa wa afya wa China walisema virusi hivyo hueda vikazaana na kusambaa katika maeneo mbalimbali duniani.

Maofisa hao walionya juu ya kusambaa kwa virusi huku wakitoa tahadhari, wakiongeza juhudi za kudhibiti maambukizi ya virusi hivyo.

Ugonjwa huo uligundulika nchini China hivi karibuni na wataalamu wa afya bado wanaendelea na kupata tiba yake, hadi sasa umeshaua watu huku wengi wakiendelea kuugua.

Idadi ya waliofariki kutokana na ugonjwa unaosababishwa na virusi hivyo imeongezeka na kufikia tisa huku watu wengine 440 wakithibitishwa kuugua.

Ofisa wa Tume ya Kitaifa ya Afya alikiri kuwa nchi hiyo kwa sasa iko katika awamu muhimu ya kuzuia na kudhibiti kusambaa kwake.

Juzi, mamlaka ilithibitisha usambazaji wa virusi hivyo kupitia binadamu.

Katika taarifa ya kwanza kwa umma tangu mwanzo wa mlipuko wa ugonjwa huo, Naibu Waziri wa Tume ya Afya ya China, Li Bin alisema kuna ushahidi kuwa ugonjwa huo unasambazwa kupitia mirija ya kutoa pumzi. Lakini China haijafanikiwa kubaini chanzo halisi cha virusi hivyo. **BBC**

# Shahidi kesi ya kina Mbowe adai kupigwa risasi na polisi

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa 12 katika kesi ya uchochezi dhidi ya vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiwamo Mwenyekiti Taifa Freeman Mbowe, Aida Ulomi (50) amedai mahakamani kwamba Februari 16, 2018 alipigwa risasi na askari polisi wakati wa ufungaji wa kampeni za uchaguzi wa mdogo wa ubunge Jimbo la Kinondoni.

Mbali na kupigwa risasi, alidai kuwa alikamatwa na kukaa mahabusu katika kituo cha Polisi Osterbay kwa siku 14 wakati akiwa majeruhi.

Shahidi huyo alitoa madai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Akiongozwa na wakili wa utetezi, Peter Kibatala, shahidi huyo alidai siku ya tukio alitoka kwenye makazi yake, Kigamboni Kisiwani, Kata ya Vijibweni, kwenda nyumbani kwa mama yake mdogo eneo la Mtaa wa Lunguya, Kinondoni kumsalimia kwa sababu alikuwa mgonjwa.

"Nilipofika nilimsalimia mama mdogo na kumsaidia baadhi ya kazi. Ilipofika saa 12:45 jioni, niliaga nikatoka kwenda kutafuta usafiri kituo cha daladala cha Kinondoni Studio kwa ajili ya kurudi nyumbani kwangu Kigamboni.

"Nilipokuwa kituoni, ghafla yalikuja magari matatu ya polisi yaliyokuwa yakitokea upande wa Magomeni kisha askari polisi waliokuwa kwenye magari hayo wakiwa na silaha, wakaanza kushuka kwa kuruka na kuanza kupiga risasi juu," alidai.

"Niliwasikia abiria wenzangu wakisema tukimbieni jamani ni risasi za moto hizo, ndipo nami nikajua kuwa ni risasi na nilipoona watu wanakimbia na mimi nikaanza kukimbia kuelekea kwenye jengo la Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kujiokoa," aliongeza Ulomi.

Alidai kabla hajalifikia jengo hilo la CCM, alishtukia amepigwa na kitu kizito mguuni na damu zikaanza kuvuja, ndipo wenzake wakamwambia kuwa ameshapigwa risasi. Shahidi huyo anayewatetea vigogo wa Chadema, alidai kuwa alikaa chini pale na muda kidogo wakafika askari polisi wanne wanaume wakamtuhumu kuwa alikuwa kwenye maandamano na kisha kuanza kumpiga, lakini alijitetea kwamba mbona haelewi kinachoendelea lakini hawakumsikiliza.

"Wale askari walimwita askari polisi wa kike ili anichukue lakini kabla ya kufanya hivyo, walikwenda kuwachukua watu waliokuwa wamekimbia na kuingia katika jengo la CCM. Kabla ya kuondoka kuna afande mmoja ambaye nafikiria alikuwa bosi wao, aliwaambia askari kuwa yameshatokea maafa hivyo waokote maganda yote ya risasi yaliyoko katika eneo hilo," alidai Ulomi.

Alidai walipomaliza kuyaokota maganda hayo afande huyo aliwaambia maafande wambebe na kumwingiza ndani ya gari na kuongeza kuwa wakati hayo yote yanatokea kidonda chake kilikuwa kinavuja damu na hakuna huduma yoyote ya kwanza aliyopatiwa.

Alidai kuwa waliofika kituoni hapo, zaidi ya polisi 10 walianza kuwapiga watu hao aliokuwa nao kwa kutumia ngumi na fimbo na kisha baadaye kuwaambia waimbe wimbo unaoitwa 'Magufuli amechukua ameweka waaa, Makonda amechukua ameweka waaa'.

"Alikuja mwanaume mmoja akiwa amevaa shati la kijani alitoa karatasi iliyokuwa na orodha ya majina ambayo yalianza kuitwa na yalipoisha, askari mmoja alimwambia tayari watu wako wameisha akajibu ndio na kuondoka na wale watu wengine waliobaki walikuwa wanataka fedha na kuwapatia askari na kisha kuachiwa," alidai.

"Wale askari waliniambia kama nina hela nitoe ili niachiwe nikawaeleza kuwa sina hata shilingi na ilipofika saa mbili asubuhi, mume wangu akaja akaomba kuniona na aliponiona nilivyoumia aliwaomba maafande waliokuwapo mapokezi wanipeleke hospitalini lakini walikataa na kusema watanipeleka wao wenyewe," alidai Ulomi.

Alidai alitibiwa katika Hospitali ya Kituo cha Polisi Osterbay na alikaa mahabusu kwa siku 14 mpaka alipomaliza sindano alizokuwa anachomwa.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya na Dk. Vincent Mashinji.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji jinai kati ya Februari Mosi na 16, 2018, jijini Dar es Salaam.

# Nec yaanza kuboresha daftari Tanga, Morogoro

**Na Juster Prudence**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeanza uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika mikoa ya Tanga na Morogoro (Halmashauri za wilaya za Ulanga na Malinyi).

Maboresho hayo yataanza Januari 23, mwaka huu na litaendelea hadi Januari 2020.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na NEC, uboreshaji huu unawahusu raia wa Tanzania ambao wametimiza umri wa miaka18.

Wengine ni waliotimiza umri wa miaka 18 siku ya uchaguzi mkuu Oktoba 2020, waliohama kutoka maeneo yao ya awali na kuhamia maeneo mengine ya uchaguzi na wale ambao kadi zao zimeharibika au kupotea.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa uboreshaji litahusisha kuondolewa kwenye daftari hilo waliofariki.

Aidha, taarifa hiyo ilibainisha kuwa uboreshaji wa daftari hilo umekamilika kwenye mikoa 25 ya Tanzania Bara na Zanzibar.




Meneja Mkazi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa DTB –Tanzania, Viju Cherian, akizungumza na mameneja wa matawi na maendeleo ya biashara katika mkutano wa 12 wa mwaka wa mpango kazi wa benki hiyo, uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: DTB**

# Miradi ya NHC yamkuna Naibu Waziri

**Na Munir Shemweta, MPANDA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Mkoa wa Katavi kwa kuwa na miradi mingi ya shirika hilo.

Dk. Mabula alitoa pongezi hizo juzi wakati akikagua miradi ya NHC kwenye mkoa wa Katavi akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na ujenzi wa miradi inayotekelezwa na shirika hilo.

Miradi aliyoikagua Naibu Waziri Mabula ni ujenzi wa nyumba za watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, ofisi na nyumba ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda.

Pia alikagua mradi wa nyumba 70 za Ilembo ambao nyumba 10 kati ya hizo ziliuzwa na zingine 60 zimepangishwa.

Alisema Mkoa wa Katavi unaweza kuwa mkoa wa kwanza au wa pili kwa kuwa na miradi mingi ya NHC na hali hiyo si tu inaonesha shirika lilivyo makini kwenye uwekezaji miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa nyumba za kuuza, kupangisha na majengo ya biashara bali inalifanya kuimarika kimkoa.

Kuhusu mradi wa jengo la biashara la Paradise lililoko Manispaa ya Mpanda, Dk. Mabula alilisifu jengo hilo kwa kuwa na mazingira mazuri ya kibiashara na kushauri taasisi za serikali katika Mkoa wa Katavi kutumia fursa ya kupanga na kuwekeza kwenye jengo hilo kwa kuwa gharama zake ni nafuu.

Aidha, aliitaka NHC Mkoa wa Katavi kuhakikisha inalitangaza jengo hilo kwa lengo la kuvutia wateja kupanga hasa ikizingatiwa kutolitangaza kunaweza kusababisha kukosa wateja.

Mabula alisema hayo baada ya kuelezwa na Kaimu Meneja wa NHC Mkoa wa Katavi na Rukwa, Masumbuko Majaliwa, kuwa mpaka sasa jengo hilo limepangisha asilimia 30 tu ya wateja.

"Mrudi kwenye kutangaza miradi yenu kupitia kipindi cha Maisha ni Nyumba na ikiwezekana kazi hiyo ifanyike mkoa kwa mkoa na mhakikishe miradi yenu mnaifanya kwa kasi, viwango na wakati ili kujenga 'trust' (uaminifu) kwa wateja," alisema.

Meneja Mawasiliano wa NHC, Muungano Saguya, alisema kwa sasa shirika linafanya vizuri katika masuala ya ujenzi jambo lililosababisha kuaminiwa na serikali.

Alisema katika mji wa serikali eneo la Mtumba, Dodoma, lilijenga majengo ya wizara nne na sasa linaendelea na utekelezaji wa miradi mingine kama vile ujenzi wa nyumba na ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) nchi nzima.

Awali, Majaliwa alimweleza Naibu Waziri kuwa kwa sasa NHC Mkoa wa Katavi na Rukwa inatekeleza miradi mbalimbali katika mikoa ya Katavi na Rukwa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu**:0714404491/0746995144**

**WAHUDUMU WA HOTELI WANAHITAJIKA,** Hoteli ndogo Bagamoyo inatafuta wahudumu, wapishi, usafi, bartender wenye vyeti. **Piga 0757 129 546.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO


### KUPOTEA KWA CHETI



**ASHA SELEMANI MKAMILE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Kilichotolewa kwa mtahiniwa namba **S.0312/0013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2013 katika shule ya sekondari ya Highlands.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi.

**RB. NA; IRI/IRI/439820/2019.**

215596702

### KUPOTEA KWA KADI

**MSAMIRU KASSIM KAABUKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji aina ya **TVS** yenye namba ya usajili **MC160CAM** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **KW/RB//17/2020**

115596902

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Emmanuel Mbeyanje** Mwampamba anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.269 DHH** aina ya Mitsubish Fuso ya Multcolour, Engine namba **Z172HB,** Chassis namba **FM657NB00197.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/73089/2020.**

115596802

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;20/2020

Ombi la **FATUMA BAKARI MGHAMBA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MERY BAKARI MGHAMBA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 14/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/01/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MOROGORO

215596402


NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MOURINHO ALIA NA UHABA WA STRAIKA

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesema uhaba wa mshambuliaji Tottenham unamlazimisha yeye "kufikiri, kufikiri na kufikiri zaidi" lakini akasema amebakia mtulivu kwenye shughuli ya soko la usajili linaloendelea.

Kwa kukosekana kwa Harry Kane kutokana na kuwa majeruhi, Dele Alli na Son Heung-Min walifunga na kuiweka mbele Spurs kwa mabao 2-1 dhidi ya Norwich City nyumbani juzi Jumatano, ingawa hawakutengeneza nafasi zaidi.

Mourinho alipatwa na pigo jingine wakati Harry Winks alipoumia na amebainisha kwamba hakuwa na chaguo jingine pale benchi wakati wakati Norwich ikisawazisha kupitia kwa Teemu Pukki kwa mkwaju wa penalti dakika ya 70 kabla ya Son Heung-Min kutupia la ushindi dakika tisa baadaye.

"Ni muhimu zaidi kwa upande wetu kupata ushindi dhidi ya timu ngumu," alisema Mourinho akiiambia BBC Sport.

"Tulikuwa na wakati mgumu kipindi cha pili na sisi wenyewe ndio wa kujilaumu.

"Tuko kwenye hali ambayo inafanya nifikiri, nifikiri na kufikiri zaidi. Niliangalia benchi na hakukuwa na mshambuliaji. Nililazimika kumtoa nje Erik Lamela kwa sababu ya kuchoka, lakini tulionyesha mchezo mzuri kwa bao letu la pili.

"Wakati Chelsea inataka ushindi, wanamwingiza Michy Batshuayi. Wakati Manchester City wakitaka kumbadilisha Gabriel Jesus, wanamwingiza Sergio Aguero.

# Klopp amkuna mmiliki Liverpool

**LIVERPOOL,** England

JOHN W. Henry ameonyesha kufurahishwa zaidi na kazi ya kocha Jurgen Klopp hasa baada ya timu hiyo kuwafunga wapinzani wao wakubwa kwenye soka la England, Manchester United, Jumapili iliyopita.


Klopp amekuwa na wakati mzuri zaidi pale Liverpool huku kichapo alichowapa Man United kikiwafanya wasogelee kabisa ubingwa wa Ligi Kuu England ambao utakuwa wa kwanza kwao kwenye historia ya klabu hiyo tangu mwaka 1990.

Mabao ya Virgil van Dijk na Mohamed Salah waliyofunga kwenye kila kipindi yamewafanya Liverpool kushinda 2-0 na kuweka pengo la pointi 16 kileleni kabla ya Manchester City hawajacheza na Sheffield United jana Alhamisi kuwakabili Wolves.

Baada ya mechi hiyo iliyopigwa Anfield, mashabiki wa Liverpool walisikika wakiimba "Tunakwenda kuchukua taji la ligi" wakati huo wachezaji wa timu hiyo walikuwa wakitoka uwanjani kuelekea vyumbani.

Wakiwa kwenye korido la Anfield, Klopp alipewa pongezi na watu mbalimbali akiwamo mmiliki wa timu, John W Henry, ambaye alimvuta na kumkumbatia, kisha kumwambia: "Safi sana. Safi kweli kweli."

Liverpool wamebakiza hatua chache tu kuelekea kulibeba taji la Ligi Kuu England msimu huu ambalo litakuwa la kwanza kwenye historia yao tangu 1990. Lakini, Klopp alisema yeye na wachezaji wake hawawezi kubweteka na wataendelea kukaza hadi mwishoni mwa msimu.





# *Pochettino wakati wowote kutua Utd*

**MANCHESTER,** England

MAURICIO Pochettino wakati wowote anaweza kutangazwa kuwa kocha mpya wa Manchester United, kwa mujibu wa ESPN.

Kocha huyo anatajwa kwamba yupo kwenye mazungumzo na 'Mashetani Wekundu' hao kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer pale Old Trafford.

Raia huyo wa Argentina amekuwa akihusishwa na kwenda kukalia kiti cha moto pale Old Trafford baada ya kufutwa kazi Tottenham Hotspur, Novemba mwaka jana.

Iliaminika pia angeenda kuchukua mikoba ya kuinoa Manchester United wakati Jose Mourinho alipofutwa kazi Desemba 2018, lakini wababe hao wa Manchester waliamua kumchukua jumla Solskjaer baada ya kuwaonyesha kiwango bora kwenye mechi zake za kwanza alipokuwa kocha wa muda.

Lakini, sasa mabosi wa Man United wanafikiria kufanya uamuzi sahihi baada ya timu kutokuwa na matokeo yanayoeleweka.

Taarifa za kutoka ndani ya klabu hiyo zinadai kwamba Man United wameshaanza mazungumzo na Pochettino, ambaye pia yupo tayari kwenda kupiga mzigo huko Old Trafford.

Man United ya Solskjaer imekuwa haieleweki kiwango chake cha uwanjani na jambo hilo ndilo linalodaiwa kuwafanya mabosi wa miamba hiyo kufikiria kumleta mtu atakayekuja kuleta mambo matamu.

Kocha mwingine anayedaiwa kwamba anaweza kufikiriwa kwa haraka kwenda kumbadili Solskjaer ni Mtaliano, Max Allegri.

HABARI MICHEZO

# Zinedine Zidane angojewa ukocha Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

UFARANSA itamwania Zinedine Zidane kuwa mrithi wa Didier Deschamps wakati kocha huyo mshindi wa dunia atakapoondoka, Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), Noel Le Graet amebainisha.

Kocha huyo wa Real Madrid awali alihusishwa na mpango wa kupewa timu ya Taifa ya Ufaransa, lakini alirudi tena kule Santiago Bernabeu mwaka jana.

Wakati huo huo, Deschamps, ambaye amekuwa kwenye kiti hicho tangu mwaka 2012, na mwezi uliopita alisaini kuongeza mkataba wake utakaomfanya akae hapo hadi wakati wa Kombe la Dunia mwaka 2022.

Kocha huyo pia alimtaja mchezaji mwenzake huyo wa zamani kama ndiye kocha ajae wa Les Bleus, na sasa Le Graet pia amempa nafasi hiyo.

"Siku ambayo Didier ataamua kuondoka au mkataba wake kutoongezwa, na kama Zidane atakuwapo, yeye ndiye atachukua nafasi hiyo," amesema Le Graet akiiambia Canal+.

Nafasi inaweza kuwapo haraka baada ya Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, wakati Deschamps muda wake utakapokuwa umefikia mwisho.

"Kuna Qatar," alisema Le Graet. "Didier atakuwa pale na halafu baada ya hapo sijui kitakachotokea."

Deschamps na Zidane walishinda Kombe la Dunia mwaka 1998 wakiwa pamoja kama wachezaji, kabla ya kocha huyo wa zamani wa Juventus kuiongoza nchi yake kutwaa Kombe la Dunia miaka miwili iliyopita nchini Urusi.





# SARRI AITAKA JUVE IIMARIKE ZAIDI

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri ameonyesha kuridhishwa na kiwango cha Juventus, lakini amebainisha kwamba timu hiyo lazima iwe bora zaidi kuliko misimu iliyopita kama wanataka kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Bianconeri hao waliwafunga AS Roma mabao 3-1 kwenye robo fainali ya Kombe la Coppa Italia Jumatano, mabao yake yakifungwa na Cristiano Ronaldo, Rodrigo Bentancur na Leonardo Bonucci kabla ya mapumziko.

Ulikuwa ni ushidi wa tano mfululizo katika mashindano yote kwa Juve, wakati ambao sasa wanaongoza kwa pointi nne kileleni mwa msimamo dhidi ya Inter Milan.

Sarri alishuhudia timu yake ikicheza kwa kujituma zaidi dhidi ya Roma, lakini akabainisha kwamba timu hiyo inahitaji kuimarika zaidi ili kuwazidi Nerazzurri na Lazio.

"Kushinda limekuwa jambo la kawaida," alielezea Sarri baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari. "Nina furaha juu yao.

"Lakini hatutakiwi kuangalia namba kwa sababu utakuwa mwaka mgumu zaidi. Tunachotakiwa kufanya ni kuwa bora zaidi kuliko misimu iliyopita kama tunataka kuleta ushindani kwenye ligi."

Ronaldo aliingia mwaka 2020 kwa kufunga mabao saba katika mechi nane na Sarri amesifia kiwango cha mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno.

# *Fati atapewa nafasi zaidi Barca- Setien*

**BARCELONA,** Hispania

ANSU Fati atapata nafasi zaidi ya kuanza "kama tu akiendelea kuimarika", amesema kocha Quique Setien baada ya Barcelona kupata ushindi kwenye mchezo wa Copa del Rey dhidi ya Ibiza.

Setien aliwapumzisha wachezaji kama Lionel Messi, Sergio Busquets na Gerard Pique kwenye mchezo huo wa Jumatano dhidi ya timu hiyo ya Daraja la Pili, ambayo ilianza kuwashangaza vinara hao wa LaLiga kwa kupata bao la kuongoza dakika ya tisa.

Iliwachukua dakika 72 Barcelona kusawazisha kupitia kwa Antoine Griezmann na baadaye akafunga la ushindi zikiwa zimesalia dakika nne mpira kumalizika.

Fati mwenye umri 17, alifunga mabao dhidi ya Osasuna na Valencia mapema msimu huu na alifunga la ushindi dhidi ya Inter Milan kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi uliopita, lakini alichangia kidogo kwenye ushindi wa 2-1 dhidi ya Ibiza.

Licha ya kutokuonyesha kiwango kizuri kwenye mchezo huo, Fati atapewa nafasi zaidi kwa kujiimarisha yeye mwenyewe kwa mujibu wa Setien.

"Kitu cha kwanza tunachokifanya ni kuangalia wachezaji tofauti kwenye nafasi tofauti," alisema Setien akiwaambia waandishi wa habari.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MENDES ATHIBITISHA FERNANDES KUTUA UTD

●●● Inaelezwa tayari Manchester United imetoa ofa kwa Fernandes, ambayo imekubaliwa...

**MANCHESTER,** England

JORGE Mendes amesisitiza kuwa hana uhakika kama Bruno Fernandes atakuwa mchezaji wa Manchester United mwezi huu, lakini wakala huyo maarufu anaamini kuwa nyota huyo wa Ureno atapata uhamisho wake mapema badala ya baadaye.

Mendes alizungumza na Sky Sports mapema jana ambapo alidai kwamba kuna uhakika wa kiungo huyo kubaki Sporting Lisbon kwa kipindi kilichobaki cha msimu.

Wakala huyo, Mendes alisema: "Sijui nini kitatokea kwa Bruno, ukweli sijui. kama ataondoka sasa, kwa uhakika ataondoka majira ya joto."

**"Sporting imekuwa ikizungumza na klabu nyingine, sina uhakika nini kitatokea kama ataondoka sasa ama mwishoni mwa msimu."**

Hata hivyo, inaelezwa tayari Manchester United imetoa ofa kwa Fernandes, ambayo imekubaliwa.

Kwa mujibu wa taarifa, 'Mashetani Wekundu' hao wameboresha ofa yao kwa Fernandes hadi euro milioni 55 pamoja na nyongeza ya bonasi ya euro milioni 10.

Ofa hii kiuhalisia ni kubwa kuliko ile ya hivi karibuni ya euro milioni 47 ambayo ilikataliwa na miamba hiyo ya Ureno. Hata hivyo, Sporting Lisbon kwa sasa inataka euro milioni 68 kwa mchezaji huyo kiasi ambacho miamba hiyo ya Old Trafford imekataa kukilipa.

Hali hiyo imemkosesha raha Fernandes na kukasirika kwa mbinu za Sporting. Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno aliweka wazi nia yake ya kuondoka klabuni hapo mwezi huu, lakini suala la euro milioni 5-10 limemkosesha nafasi ya kucheza Ligi Kuu England.

## ZISIKUPITE

### YAKWAMA KWA AUBAMEYANG

BARCELONA inahaha kukamilisha dili la mkopo kwa mshambuliaji wa Valencia, Mhispania Rodrigo Moreno, 28, tayari imekwama katika mpango wake kama huo kwa straika wa Arsenal, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30. ***(Sport)***

### SPUR, JOSE MAZUNGUMZONI

TOTTENHAM inamuwinda mshambuliaji wa Real Sociedad, Mbrazil Willian Jose na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kwa sasa yupo London kwa mazungumzo. ***(AS)***

### YAMKOMALIA EVERTON

EVERTON bado inavutiwa na mshambuliaji wa Gremio, Mbrazil Everton Soares, 23. ***(UOL, via Star)***

### KURZAWA ANUKIA ARSENAL

PSG inataka angalau pauni milioni 4.2 kutoka Arsenal ambayo inavutiwa na huduma ya beki Mfaransa Layvin Kurzawa, 27, mwezi huu. Beki huyo wa pembeni atakuwa nje ya mkataba majira ya joto. ***(Telegraph)***

### REAL KUMREJESHA BALE SPURS

REAL Madrid inajiandaa kujadili kurejea Tottenhm kwa nyota wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 30, Tottenham lakini ina wasiwasi juu ya muundo wa dili lolote. ***(Telegraph)***

### KUMREJESHA VESTERGAARD

LEICESTER City inakaribia kukamilisha dili la kumrejesha beki wa kati wa Southampton, Jannik Vestergaard, 27, baada ya kutoa ofa ya pauni milioni 15 kwa nyota huyo wa kimataifa wa Denmark. ***(Sun)***

### KUACHANA NA COUTINHO

BAYERN Munich haitashughulika na nafasi ya iliyopewa ya kumsajili jumla kiungo Mbrazil Philippe Coutinho, 27, anayeichezea kwa mkopo kutoka Barcelona. ***(Bild, via Mirror)***

### MARTINELLI KUJAZWA MIHERA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Gabriel Martinelli anajiandaa kuongezewa mshahara mara tatu ya ule anaolipwa ifikapo mwisho wa mwezi wakati huu Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 18 akiwa anatupiwa jicho na miamba ya Hispania, Real Madrid.***(Mail)***

### CAVANI WA ATLETICO- BABA

BABA wa mshambuliaji wa PSG, Edinson Cavani, mzee Cavani amesema mshambuliaji huyo atajiunga na Atletico Madrid kama klabu hiyo itakubaliana ofa yake na miamba hiyo ya Ufaransa. ***(Guardian)***

### HATIHATI KWA GUIMARAES

ARSENAL imekuwa ikihusishwa na kiungo mkabaji wa Athletico Paranaense, Bruno Guimaraes lakini Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 22, anajiandaa kujiunga na Lyon ya Ufaransa. ***(L'Equipe, via Mirror)***

### YAJITOSA KWA CAVANI

CHELSEA imetoa ofa ya kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Uruguay, Edinson Cavani, 32, kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu. ***(Times)***

## Shime aipania Burundi U-17

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17, Bakari Shime, amesema wanakwenda Burundi kumalizia kazi waliyoianza jijini Dar es Salaam ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini India.

Kikosi cha Tanzania kiliondoka nchini jana na kuwasili salama mjini Bujumbura kwa ajili ya mchezo wa marudiano unaotarajiwa kuchezwa kesho nchini humo.

Tanzania itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 5-1 walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa wiki mbili zilizopita jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana kabla ya kuondoka nchini, Shime alisema kuwa kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na wanakwenda huko wakiwa na malengo ya kusaka ushindi wa pili.

Shime alisema anaamini matokeo ya ushindi ndio yatawavusha wakiwa na nguvu na kamwe hawatabweteka na matokeo waliyopata katika mechi ya kwanza. Alisema mshambuliaji wake tegemeo, Aisha Masaka ambaye aliumia mguu anaendelea vema na juzi alifanya mazoezi pamoja na wenzake, hivyo wasiwasi wa kumkosa katika mechi hiyo ya marudiano umemalizika.

Endapo Tanzania itasonga mbele, itakutana na mshindi kati ya Ethiopia au Uganda. Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Kampala wenyeji walipata ushindi wa mabao 2-0 na marudiano yanatarajiwa kufanyika kesho mjini Addis Ababa.

## Kipanga yajipanga kubeba FA Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kipanga imesema imejipanga kuhakikisha inasonga mbele katika michuano ya Kombe la FA ili waweze kuwa wawakilishi wa Zanzibar katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Kipanga itashuka dimbani leo kuwania kombe hilo la FA kwa kuvaana na timu ya Kilimani City inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Msaidizi wa Kipanga, inayocheza Ligi Kuu Zanzibar, Maulid Othman, alisema kuelekea mechi hiyo itakayochezwa katika Uwanja wa Mau, wamejiandaa vizuri ili kuhakikisha wanatoka na ushindi utakaowapeleka mzunguko wa pili wa hatua ya 16 ya michuano hiyo.

"Timu imejiandaa Ili kuhakikisha inatoka na ushindi japokuwa hatukuweka kambi kwa ajili ya FA lakini hadi sasa wachezaji wapo vizuri na hakuna majeruhi, naimani tutashinda tu," alisema.

Michuano ya FA imeshirikisha timu 32 ikiwamo 11 za Ligi Kuu ya Zanzibar zilizopo katika Kisiwa cha Unguja na tatu kutoka kila mikoa miwili ya Unguja huku Mkoa wa Mjini Magharibi wenyewe ukitoa timu mbili.

# NSANZUWIMO ABEBA LAWAMA KIPIGO YANGA

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

KOCHA Mkuu wa Singida United, Ramadhan Nsanzuwimo, amesema anakubali kubeba lawama zote kufuatia kikosi chake kupoteza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga uliochezwa juzi mkoani hapa.

**Singida United ambayo iko katika hatari ya kushuka daraja, ilichapwa mabao 3-1 na Yanga licha ya kufanya usajili wa wachezaji 13 wapya katika dirisha dogo lililofungwa hivi karibuni.**

Kocha Nsanzuwimo alisema uamuzi wake wa kubadili wachezaji watano katika kikosi cha kwanza ndio uliwaumiza na anakiri walicheza vibaya kwenye mchezo huo wa nyumbani.

"Nakubali kubeba lawama za matokeo haya, nilibadilisha wachezaji watano wa kikosi cha kwanza ambao walipata ushindi katika mchezo uliopita dhidi ya Ruvu Shooting bila sababu za msingi, lakini pia 'fitnesi' yetu leo (juzi) ilikuwa chini sana, mipira ya kasi hatukuweza kuipata, hatukucheza kitimu," alisema Nsanzurwimo.

Kocha huyo aliongeza kuwa safu yake ya ulinzi ya kati haikuwa vizuri katika mchezo huo, lakini akampongeza golikipa wake Obren Chaima kwa kazi nzuri ya kuokoa hatari langoni mwake na kupunguza idadi ya mabao ya kufungwa.

"Wachezaji wangu hawakucheza kwa kuelewana, tulifungua sana mchezo, tulikuwa na nidhamu mbaya, safu ya ulinzi ilikuwa na shida, lakini bado nasisitaza nawajibika kwa matokeo, tutayafanyia kazi makosa na tutarejea kwenye ushindani katika mechi zinazofuata," Nsanzurwimo alisema.

Naye beki wa pembeni wa timu hiyo, Haji Mgwali, alisema bado kikosi chao kinajengwa na endapo wataelewana, Singida United itaanza kupata matokeo mazuri.

"Timu yetu bado inaungaunga, kocha anaendelea kukijenga kikosi, ninapenda kuwaambia mashabiki wa Singida United wasivunjike moyo, tupo vizuri, mechi bado ni nyingi, nafasi ya kubadilisha upepo tunayo na tutabakia katika Ligi Kuu," alisema Mgwali, beki wa zamani wa Yanga.

Singida United ambayo ilishatolewa katika mashindano ya Kombe la FA, itaendelea na mazoezi yake kwa ajili ya kuwafuata Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Februari Mosi kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

**ZUHMNA...**



Baadhi ya wachezaji wa mchezo wa Zuhmna, wakifanya mazoezi ya mchezo huo katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Niyonzima: Mapambano Yanga yameanza*

**Na Somoe Ng'itu,** SINGIDA

KIUNGO wa kimataifa wa Yanga kutoka Rwanda, Haruna Niyonzima, amesema ushindi ambao wameupata juzi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida United ni ishara ya kikosi hicho kuelekea katika mafanikio ambayo wanayahitaji.

Niyonzima alifunga bao la pili katika ushindi wa mabao 3-1, huku la kwanza likipachikwa na David Molinga 'Falcao' na lingine likiwekwa kimiani na mshambuliaji Mghana Yikpe Ghislain.

Akizungumza na gazeti hili jana, Niyonzima alisema kikosi chao kina wachezaji wazuri na kitakapozoeana vema, kitakuwa 'moto' na anaamini watafikia malengo waliyonayo ya kufanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano mengine watakayoshiriki.

Kiungo huyo ambaye aliwahi kuichezea Simba misimu miwili iliyopita akitokea Yanga, alisema ligi bado haijafika mwisho na ari waliyonayo wachezaji wa timu hiyo, watamaliza msimu katika nafasi nzuri na itakayowapa furaha.

"Hii ni Yanga mpya, haijazoeana kama watu wanavyoijua, lakini tukizoeana tutakuwa vizuri zaidi, siwezi kusema gari limewaka, naweza kusema hii ni 'starter' nzuri," alisema kiungo huyo wa zamani wa APR na AS Kigali zinazoshiriki Ligi Kuu Rwanda. Aliongeza kwa kuwaomba Wanayanga wote kuimarisha umoja na ushirikiano ili timu iwe na kazi rahisi ya kufikia malengo na hakuna kisichowezekana katika soka.

"Hatujakata tamaa bado, tutapambana katika kila mechi tutakayocheza, lakini ninawaomba mashabiki, viongozi, wachezaji na wadhamini wetu tuendelee kuwa na mshikamano, tusaidiane, Yanga tutafikia malengo tunayoyahitaji wote," Niyonzima alisema.

Baada ya kurejea Yanga akitokea AS Kigali, Niyonzima alipangwa katika kikosi cha kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya watani zao Simba ambayo ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2 na alishuhudia wakifungwa dhidi ya Kagera Sugar (3-0) na wakipoteza pia walipocheza dhidi ya Azam FC (1-0).

Yanga sasa itajiandaa kuwakaribisha 'Maafande' wa Tanzania Prisons katika mechi ya raundi ya nne ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Michezo
Ijumaa Januari 24, 2020
Nipashe



Mendes athibitisha Fernandes kutua Utd HABARI UK.30

# Eymael afunguka usajili mpya Yanga

●●● Akunwa na vitu vya Mghana Morrison, ataja wengine wawili huku akiichambua Singida United kwa...

**Na Somoe Ng'itu,** SINDIGA

LICHA ya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Singida United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael amesema haikuwa kazi rahisi kupata pointi tatu katika mchezo huo uliochezwa juzi mkoani hapa huku akiweka wazi kuhusu usajili mpya klabuni hapo.

**Ushindi huo ulikuwa wa kwanza kwa Mbelgiji huyo ambaye amechukua mikoba ya Mwinyi Zahera baada ya kuambulia vichapo mara mbili kutoka kwa Kagera Sugar na Azam FC wiki iliyopita.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Eymael alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu na yenye ushindani wakati wote na ushindi walioupata umetokana na wachezaji wake kucheza kwa kuelewana na kujituma zaidi.



Eymael (pichani) alisema wapinzani wao pia wana kikosi kizuri na kama wangekuwa makini, wangeondoka na ushindi mnono katika mchezo huo uliochezeshwa na refa Omary Mdoe.

"Ilikuwa ni mechi ngumu kama nilivyosema kabla ya kuanza, haikuwa rahisi, hata tulipokuwa mbele kwa bao 1-0, ushindani ulikuwa mkubwa, lakini tulipoteza nafasi nyingi za kufunga, ikiwamo ile ya kubakia na kipa tu," alisema Eymael.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa anawapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha mabadiliko katika mechi hiyo na hali hiyo ilisaidia kupata matokeo chanya ambayo walikuwa wakiyahitaji zaidi baada ya kurekebisha makosa waliyofanya katika mechi mbili zilizopita.

"Tulikuwa na muunganiko mzuri, walicheza vizuri, pia wachezaji wapya walisaidia kuongeza nguvu katika mechi hiyo, lakini napenda kuwapongeza wapinzani wangu kwa changamoto waliyotuonyesha, wana kikosi kizuri na ninawaombea kheri wasishuke daraja," Mbelgiji huyo alisema.

Hata hivyo, Eymael alisema kama angewahi kutua Yanga kabla ya dirisha la usajili halijafungwa, angesajili nyota wapya wawili ili kuongezea nguvu katika kikosi hicho.

"Huwa sipendi kuzungumzia mchezaji mmoja mmoja, ila Bernard (Morrison) ni mchezaji mzuri na ameonyesha uwezo wake katika mechi yake ya kwanza, lakini naamini atatusaidia, ila nilichelewa kutua, kama ningewahi mapema kabla usajili haujamalizika, ningeongeza mchezaji mmoja au wawili katika kikosi changu," Eymael aliongeza.

Yanga ambayo ina pointi 28, imepaa hadi katika nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kucheza mechi 15 wakati wapinzani wao, Simba wenye pointi 41 wakiendelea kukaa kileleni lakini wakiwa mbele mechi moja.

Kikosi hicho cha Jangwani kilitarajiwa kurejea jijini Dar es Salaam jana jioni kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kuivaa Tanzania Prisons katika mechi ya Kombe la FA inayotarajiwa kuchezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Uhuru wakati vinara wa Ligi Kuu Bara, Simba wao watawakaribisha Mwadui FC kesho kwenye uwanja huo huo.

KIPIGO...



Antoine Griezmann akiifungia Barcelona moja kati ya mabao mawili aliyofunga wakati wakitokea nyuma na kushinda 2-1 dakika ya 72 na 90+5 kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Mfalme (Copa del Rey) dhidi ya Ibiza ya Segunda B, mchezo ukipigwa katika Uwanja wa Manispaa ya Can Misses juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Wababe wa Simba waitisha FA

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Simba ikiipeleka mechi yao ya Kombe la Shirikisho (FA Cup) katika Uwanja wa Taifa kesho, wapinzani wao Mwadui FC wamejigamba kuitupa nje kwenye michuano hiyo ambayo bingwa huiwakilisha nchi katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba jana ilitangaza kuwa mechi hiyo ya kesho itapigwa katika Uwanja wa Taifa badala ya ule wa Uhuru.

Hata hivyo, wapinzani wao wakizungumzia mchezo huo, Katibu Mkuu wa Mwadui FC, Ramadhani Kilao alisema wamejipanga vizuri kukutana na Simba, ambayo msimu huu wa Ligi Kuu imepoteza mchezo mmoja tu dhidi yao kati ya 16 iliyocheza hadi sasa.

'"Tumejipanga vizuri kukutana na Simba katika mchezo huo wa keshokutwa tunaomba mashabiki wetu waje kutusapoti," alisema.

Alisema kikosi chao kipo imara na kudai wanaiheshimu Simba kutokana na kuwa na wachezaji wengi wazuri.

"Kwa mujibu wa kocha, tutaingia kwa tahadhari tukijua tunacheza na bingwa mtetezi lengo ni kushinda,"alisema huku akishukuru kutokana na wachezaji wao wote kuwa katika hali nzuri kuelekea mechi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >